**UFASIHI SIMULIZI KATIKA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT: Mifano kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad***

**Khatib Khamis Saleh**

**Tasinifu ya Uzamili Katika Kiswahili**
**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**
**Septemba, 2015**

**UFASIHI SIMULIZI KATIKA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT: Mifano kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad***

**Na**

**Khatib Khamis Saleh**

**Tasinifu iliyowasilishwa Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili katika**

**Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**
**Septemba, 2015**

**ITHIBATI**

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo; **Ufasihi Simulizi katika Riwaya za Shaaban Robert: Mifano kutoka *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

..........................................

Dkt. Hadija Jilala

(**Msimamizi**)

**.....................................................**

**Tarehe**

## IKIRARI NA HAKI MILIKI

Mimi **Khatib Khamis Saleh,** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada yoyote.

**Saini** ..........................................................................

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## SHUKRANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenye-enzi Mungu (Allah) muumba na muweza wa kila kitu, kwa kunijaalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Namshukuru tena kwa unyenyekevu pamoja na tauhidi kwa kusema, Alhamdulillah Rabbilaalamina.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa, Msimamizi wangu Dkt. Hadija Jilala kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa pamoja na kunifunza misingi ya nadharia za fasihi, fasihi fafanuzi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe afya njema pamoja ukakamavu na amzidishie kila la kheri, na kumuepusha kila la shari, Amin. Tatu, napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu waliouonyesha kwa kuelewa kuwa nilikuwa masomoni, kwani kwa baadhi ya nyakati waliukosa upendo wa baba.

Nne, napenda kuwashukuru walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia na vitendo. Walimu hao ni Profesa E. Mbogo, Profesa T.Y. Sengo, Profesa S. Mdee, Dkt. P. Lipembe, Bwana Moh’d Omary pamoja na Bwana Bakar Kombo. Tano, napenda tena kumshukuru Mwenye-enzi Mungu, kunipa nguvu na uwezo wa kuniwezesha kuichapa kazi hii ya tasnifu na kuiwezesha kuiwasilisha kwa wakati muafaka.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, Bw. Khamis Saleh na Bibi Asha Khatib kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, kunifunza mema, kunikataza mabaya, na kunipa moyo na kuniwezesha kifkira na maadili mema katika kipindi chote cha masomo yangu, tangu darasa la kwanza mpaka sasa ninapokamilisha masomo yangu ya shahada ya Uzamili. Mawazo yao na busara zao katika elimu nitazikumbuka daima na kuwa chachu ya kujiendeleza zaidi.

Vilevile ninamtabarukia mke wangu kipenzi Zehera Abdalla Said, kwa ushawishi, uvumilivu, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa katika masomo yangu. Pia kwa msaada wa hali na mali katika kukamilisha masomo yangu, ikiwa ni pamoja na gharama za masomo na kuwa msimamizi na nguzo imara na thabiti katika kuhakikisha sikati tamaa ila ninamaliza masomo yangu, tangu shahada ya kwanza mpaka sasa shahada ya pili (Umahiri).

Ninawatabarukia pia wanangu Muhamed Khatib, Mudh-hir Khatib, Farida Khatib na Fat-hiya Khatib, pia kaka yangu Amour Khamis na wadogo zangu Saleh Khamis na Mayasa Khamis, wakwe zangu Salma Hemed na Abdalla Said pia mjomba wangu Juma Kheir, kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Ni matumaini yangu kuwa wataweza kutambua umuhimu wa elimu katika maisha ya mwanandamu ili iwe ni changamoto kwao.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru Mwalimu wangu mkuu Shehe Hassan Moh’d, kwa mchango wake wa hali na mali ikiwa ni pamoja na kuniruhusu kujiunga na masomo haya.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert kwa kutumia mifano ya riwaya: Mfano kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kufafanua vipengele vinavyojenga fasihi simulizi na jinsi vilivyotumika kuibua dhamira, na kutathmini na kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi, na namna mbinu hizo zinavyotumika kuibua dhamira za riwaya hizo.

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu, nasibu na ile ya uteuzi rahisi, wakati ambapo data zilikusanywa kwa kutumia mbinu nne, ambazo ni mapitio ya maandiko, usaili, dodoso na majadiliano ya vikundi. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Aidha nadharia ya mwingilianomatini ilitumika kukusanyia, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa, mtunzi ametumia mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wake, pamoja na kuwa kazi hizo zina mpishano katika kutungwa kwake. Aidha, riwaya zote mbili ni matokeo ya athari za mapokeo ya matumizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika, ambapo mtunzi ameathiriwa na masimulizi ya hadithi za fasihi simulizi na masimulizi ya kawaida katika utunzi wa riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

YALIYOMO

**ITHIBATI** ........................................................................................ i

**IKIRARI NA HAKI MILIKI** ........................................................................ ii

**SHUKRANI** ........................................................................................ iii

**TABARUKU** ........................................................................................ iv

**IKISIRI** ........................................................................................ ~~v~~ vi

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........................................................................ x

**SURA YA KWANZA** ........................................................................ xi~~1~~

1.0 Utangulizi: ........................................................................ xi~~1~~

1.1 Usuli wa Utafiti: ........................................................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti: ........................................................................ 6~~7~~

1.3.0 Malengo ya Utafiti ........................................................................ 7~~8~~

1.3.1 Lengo Kuu ........................................................................ **Error! Bookmark not defined.** ~~8~~

1.3.2 Malengo Mahsusi ........................................................................ 7~~8~~

1.3.3 Maswali ya Utafiti ........................................................................ 7~~8~~

1.4.0 Umuhimi wa utafiti: ........................................................................ 7~~9~~

1.4.1Mipaka ya Utafiti: ........................................................................ 8~~10~~

2.0 Dhana ya Fasihi Simulizi ........................................................................ 10~~11~~

2.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi ........................................................................ 16~~17~~

2.2.1 Semi ........................................................................ 17~~18~~

2.2.2 Mazungumzo ........................................................................ 17~~18~~

2.2.3 Masimulizi ........................................................................ 17~~18~~

2.2.4 Maigizo ........................................................................ 18~~19~~

2.2.5 Ushairi simulizi ........................................................................ 18~~19~~

2.2.7 Ngomezi ........................................................................ 20

2.3.0 Tafiti kuhusu Riwaya ya Kiswahili ........................................................................ 23~~24~~

2.4.0 Pengo la utafiti ........................................................................ 31

**SURA YA PILI**......................................................Error! Bookmark not defined.~~**32**~~

2.4.1 Kazi tangulizi ........................................................................................ 31~~32~~

3.4.2 Kiunzi cha Nadharia....................................**Error! Bookmark not defined.**~~33~~

3.4.2.1 Nadharia ya Mwingilianomatini ................................................................ 32~~36~~

2.4.3 Hitimisho............................................................................................... 34~~39~~

**SURA YA TATU**........................................................................................ **35~~40~~**

3.0 Utangulizi.................................................................................................. 35~~40~~

3.2 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli.................................................... 35~~40~~

3.1 Eneo la Utafiti ........................................................................................... 36~~41~~

3.2.1 Kundi Lengwa.......................................................................................... 37~~41~~

3.2.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu................................................................ 37~~43~~

3.2.3 Uteuzi nasibu/Mbinu bahatishi ................................................................. 40~~45~~

3.2.4 Mbinu ya uteuzi rahisi.............................................................................. 41~~45~~

3.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ..................................................................... 41~~46~~

3.3.1 Mbinu ya Maktabani ................................................................................. 42~~47~~

3.3.2 Mbinu ya Usaili.......................................................................................... 42~~47~~

3.3.3 Mbinu ya Dodoso....................................................................................... 43~~48~~

3.3.4 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi ............................................................. 44~~49~~

3.4 Zana za Utafiti................................................**Error! Bookmark not defined.**~~49~~

3.4.1 Hojaji........................................................................................................ 45~~50~~

3.4.2 Matini ...................................................................................................... 45~~50~~

3.4 Uchambuzi wa Data ..................................................................................... 46~~50~~

3.5 Hitimisho.................................................................................................... 47~~52~~

**SURA YA NNE**......................................................Error! Bookmark not defined.~~**55**~~

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA**............................................. **48~~55~~**

4.0 Utangulizi.................................................................................................. 48~~55~~

4.1 Vipengele vya fasihi simulizi katika kitabu cha *Adili na Ndguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. ...................................................................................................... 48~~56~~

4.1.2 Ufasihi simulizi katika *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad***Error! Bookmark not d**

4.2.0 Chanzo: Data za utafiti, ........ 4957
4.2.1 Ufasihi siumulizi katika Riwaya *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad*. ........ 5058
4.2.2 Mandhari ilivyoibuliwa na matumizi ya vipengele vya fasihi. ........ 5158
4.2.3 Wahusika walivyoibuliwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi. .... 5360
4.2.4 Masimulizi yalivyoibuliwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi.**Error! Bookmark no**
4.2.5 Ushairi ulivyoibuliwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi.**Error! Bookmark not def**
4.2.7 Semi ilivyoibuliwa naumizi ya vipengele vya fasihi simulizi.**Error! Bookmark not defined.**8
4.3 Hitimisho ........ 7790

**SURA YA TANO ........ 7892**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 7892**
5.0 Utangulizi ........ 7892
5.1 Muhtasari ........ **Error! Bookmark not defined.**92
5.2 Mahitimisho ya Jumla ........ **Error! Bookmark not defined.**98
5.3 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti Zijazo ........ **Error! Bookmark not defined.**99

**MAREJELEO ........ 84100**
KIAMBATISHO Na. I ........ 87103
MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WANAFUNZI WA FASIHI, WA CHUO KIKUU, SEKONDARI NA WALIOSOMA KAZI ZA MTUNZI ........ 87103
KIAMBATISHO Na. I1 ........ 88104
MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WASIMULIA HADITHI PAMOJA NA WASIKILIZA HADITHI ........ 88104
KIAMBATISHO Na. II1 ........ 89105
MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI WALIMU WA FASIHI. ........ 89105
KIAMBATISHO Na. IV ........ 90106
DODOSO KWA WALIMU WA FASIHI CHUO KIKUU HURIA KUTOKA TAASISI ZA TATAKI NA SANAA ZA MAONESHO ........ 90106
KIAMBATISHO Na. V ........ 92108
DODOSO KWA WANAFUNZI WA KOZI YA FASIHI ........ 92108

KIAMBATISHO Na. VI........................................................................................ 94~~110~~
DODOSO KWA AJILI WATU WALIOWAHI KUSOMA KAZI ZA MTUNZI 94~~110~~

**ORODHA YA MAJADWELI**

Jadweli namba 1 : Kielelezo kinachoonyesha Jumla ya vipengele vya fasihi simulizi…. ........................................................................................................ 23~~24~~

Jedwali namba 2 - Idadi ya washiriki wa utafiti ..................................................... 41~~46~~

Jadweli namba 3 - Kielelezo kinachoonyesha vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya kitabu cha *Adili na Nduguze na Wasifi wa Siti Binti Saad.* ...................... 49~~57~~

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI KWA UJUMLA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi inayobainisha usuli wa tatizo la utafiti lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Kwa hivyo, sura hii inabanisha na kueleza usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu na umuhimu wa utafiti, masuala ya maadili ambayo yalizingatiwa kabla, wakati na baada ya utafiti.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Wataalamu mbali mbali wameelezea na kufafanua maana ya riwaya. Kutokana na ukweli huo ni dhahiri kuwa kuna maoni mbali mbali yanayohusu dhana ya riwaya, Maneno ambayo yamekaririwa na watalamu wote, ni kuwa riwaya ni utanzu wa fasihi andishi, ikiwa ni pamoja na ushairi na tamthiliya.

Matteru (1976) anafafanua kuwa riwaya ni hadithi ndefu ambazo zimeandikwa. Kutokana maana hii tunaweza kuona mambo matatu makuu katika dhana ya riwaya, kwamba riwaya ni hadithi, hadithi ni lazima iwe ndefu na ni lazima iwe imeandikwa.

Mphalale (1976), anasema riwaya ni hadithi ndefu za maneno kati ya 35,000 na 50,000. Tunaweza kusema kwamba kuna riwaya ndefu na riwaya fupi, kulingana na idadi ya maneno yaliyotumiwa na mwandishi.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, riwaya ni kazi ambayo inakuwa na sifa mbali mbali, kuwepo na ubunifu, usimulizi (ni hadithi ya kisimulizi la kinathari), mpangilio au msukumo fulani wa matukio (ploti), mfungamano wa wakati, visa vinatendeka katika wakati fulani, inatakiwa iwe na maneno mengi na itakapokuwa na maneno pungufu ya elfu tatu (3000), yaweza kuitwa Novela, pawepo na mawanda mapana (kwa upande wa yale yanayozungumzwa, wakati na mahali pa matukio hayo), na pia pawepo na uchangamani katika visa, dhamira, tabia, wahusika n.k.

Senkoro (1982) na Wamitila (2002) wanaeleza kuwa riwaya ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui. Kisa ambacho urefu unaoruhusu kisa kitambe na kutambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwanadamu. Hivyo riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana, maisha ya jamii.

Kuhusiana na chimbuko au chanzo cha utanzu huu wa fasihi, wataalamu wengi au wote wanakubaliana na chanzo cha riwaya ni hali halisi ya kijamii, pia wanakubaliana kuwa utanzu huu ni mchanga, ukilinganisha na tanzu kama ushairi, michezo ya kuigiza au tamthiliya.

Ndungo na mwenzake (1991) wanasema kuwa, miongoni mwa riwaya za mwanzo kuzuka ilikuwa ni riwaya ya *Robinson Cruisoe (1719)* ya Daniel Defoe. Riwaya hii ilizuka kutokana na maendeleo na mabadiliko ya uvumbuzi wa viwanda. Ukoloni na uvumbuzi wa viwanda ulileta haja ya kueleza mambo kwa njia ya hadithi na ngano

ambazo zilikuwepo kwa wakati huo. Wanaendelea kusisitiza kuwa, kuzuka kwa miji na viwanda kulistawisha uandikaji wa riwaya na usomaji kupanuka. Maendeleo katika vipengele vyote vya maisha kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii, yalizusha haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ambao uchangamano wake wa kifani na kimaudhui ungedhibiti nyanja hizi zote.

Akijadili kuhusu kuzuka kwa riwaya Mulokozi (1996) anasema kuwa riwaya haikuzuka hivi hivi tu, bali ilitokana na fani za masimulizi (za hadithi) zilizokuwepo kabla. Hivyo fani hizo zilikuwemo katika fasihi simulizi iliyokuwepo kabla ya kuzuka utanzu wa riwaya katika fasihi andishi, na ziliigwa na watunzi wa mwanzo wa riwaya. Watunzi hao walisukumwa na mabadiliko ya kijamii ya karne ya 16-18 huko Ulaya. Fani ya jadi ambazo zilichangia katika kuchapuza riwaya ni ngano, hekaya, tendi, visa kale, historia, siasa, masimulizi ya wasafiri, insha na tafsiri.

Hoja za Ndungo mwenzake (1991) pamoja na Mulokozi (1996) zinadhihirisha kuwa, riwaya ilianzia huko Ulaya, kutokana na mabadiliko mbali mbali ya kijamii, yaliyotokea nchi za Ulaya na kuathiri wanajamii. Masimulizi yalikuwepo kabla ya mabadiliko hayo ndiyo yaliyotumika kuweza kuonya, kuburudisha, kuliwaza, kutunza historia ya jamii, kwa kutumia mfumo wa maandishi, ambapo yalikuwa ni maendeleo mapya katika dunia. Hali hii inayothibitisha kuwa fasihi ni lazima kuendana na mabadiliko ya jamii.

Mulokozi (1996) anasisitiza kuwa kufika karne ya kumi na sita (16), fani zilizotajwa kama vile ngano, hekaya, tendi, visakale, historia, insha na tafsiri, zilikuwa zimeshaenea

pia kufahamika na mataifa mengi. Hivyo kulihitaji msukumo wa jamii kiteknolojia na kiuchumi, ili ziweze kuwa za riwaya.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa, palikuwepo mambo yaliyopelekea kuenea kwa vitu hivyo ndani ya jamii. Hivyo ukuaji mkubwa wa shughuli za kiuchumi huko Ulaya. Ukuaji huo ulishikamana na biashara za masafa marefu za baharini, kutoka bara moja hadi bara jengine. Vile vile msukumo mwengine ni kuvumbuliwa kwa Mabara ya Amerika pamoja na kukua kwa vitendea kazi kazi (nyenzo) vya uzalishaji wa viwandani barani Ulaya. Hali iliyosababisha mapinduzi ya viwanda.

Chanzo cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili ni fani za kijadi ni ngano, hekaya, tendi, visa kale, historia, sira, masimulizi ya wasafiri, insha na tafsiri. Watoto na wazee walikuwa wanakutana na kutambiana hadithi kwa nia ya kushauri, kuonya, kutahadharishana na kuelezana mambo ya mbali mbali kuhusu jamii. Hadithi hizi zilipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine (tazama Ndongo na Mwai na mwenzake 1991 na Mulokozi (1996). Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa majilio ya wazungu kama majilio wa wageni waliotangulia katika nchi za Afrika ya Mashariki, yalikuwa na athari kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Kwani hati za kilatini zilianza kutumika 1890 kwa watu wa Afrika Mashariki, na yale yaliyoandikwa na waalimu wenyewe kwa kutumia mila na tamaduni za kwao. Kulikuwa hakuna yaliyoandikwa na Waafrika kwa wakati huu. Hivyo hadithi za Waafrika zilikuwa katika masimulizi.

Maelezo hayo yanathibitisha kuwa riwaya ni mazao ya fikra na mawazo ya wageni wa kizungu. Mara nyingi vitabu hivi vilikita kuelezea tajriba yao ya maisha, silka, malezi,

na mtazamo kuhusu maisha. Pia waliendelea kutunga vitabu vya hadithi vya Kiarabu na kizungu, baadhi ya vitabu hivyo ni kama *Alfu lela Ulela (1313), Safari ya Gulliver (1932, Mashimo ya Mfalme Suleiman (1929), Hekaya za Abunuasi (1915)* n.k. Waafrika walitunga hadithi kwa kutumia maudhui na mtindo katika mtiririko wa visa na mengineyo yaliyoegemea katika kuendeleza ukoloni na utamaduni wa kigeni. Riwaya ziliendelea kutungwa kwa kuziba pengo la ukosefu wa riwaya katika fasihi ya Kiswahili. Palianzishwa mashindano ya uandishi na taasisi ya kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa utungaji wa hadithi fupi pamoja na vitabu vidogo vidogo na lugha iliyotumiwa ni ile iliyokubaliwa na taasisi hiyo, na mfano wa vitabu ni *Mjomba Remus* (1935), *Safari ya Juma* (1949), *Safari ya Sungura* (1926) n.k.

Hadithi na vitabu vilivyotungwa havikusaidia ila kukuza nadharia za kuendeleza na kudumisha ukoloni na kudunisha utamaduni wa Kiafrika, ijapokuwa havikusaidia kwa kiasi fulani lakini hali hii ilipelekea kuibua waandishi wa riwaya za Kiswahili.

Maelezo hayo yanadhahirisha kuwa chanzo cha riwaya za Kiswahili, ni mchango mkubwa uliotokana na biashara na mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Hali hii ilianza Ulaya na kuja Afrika, kwa kutumia biashara ya baharini. Ambapo biashara hii ilipotokea Ulaya kuja Afrika iliathiri kwa kiasi kikubwa mila, silka na desturi za Waafrika. Hali iliyopelekea kufuata uhalisia wa Kiafrika na kuwa mchanganyiko kati ya Uafrika na Uzungu. Ndipo palipopatikana kitu kiitwacho riwaya inayotokana na fasihi andishi badala ya hadithi inayotokana na fasihi simulizi. Hata hivyo tukirejelea mwazo ya Mulokozi (1996), yanaonyesha kuwa riwaya ya Kiswahili imechimbuka katika fasihi simulizi.

Kutokana na utalii huo kuhusu riwaya na chimbuko lake. Utafiti huu unaona kuwa ipo haja kuchunguza ufasihi simulizi katika riwaya ili kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vimeingizwa katika utanzu wa riwaya kama mbinu ya kisanii inayotumika kujenga riwaya za Kiswahili. Kwa kufanya hivi tunaweza kubaini nafasi ya fasihi simulizi katika riwaya za Kiswahili. Kwa hiyo utafiti huu ulichunguza riwaya mbili za Shaaban Robert ili kubaini ufasihi simulizi uliojitokeza katika riwaya hizo.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Kama tulivyoona hapo awali kwamba chanzo cha riwaya ya Kiswahili ni fasihi simulizi, Swali linalotatiza utafiti huu ni je kuna athari yoyote ya fasihi simulizi katika riwaya za Kiswahili? Je, vipengele vya fasihi simulizi hujitokeza katika riwaya za Kiswahili? Kutokana na maswali hayo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika riwaya za Shaabn Robert ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad*, ili kubaini jinsi vipengele vipi vya fasihi simulizi vilivyotumiwa na mtunzi kama mali ghafi ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili.

## 1.3.0 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya jumla (kuu) na malengo mahsusi. Kama yanavyojionyesha katika sehemu ifuatayo;

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kuchunguza ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert kwa kutumia mifano ya riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anatumia vipengele vya fasihi simulizi kama mali ghafi ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahsusi mawili.

1) Kubaini vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*
2) Kubainisha dhamira zinavyowasilishwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

1) Je, ni vipengele vipi vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad?*
2) Je matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya ya *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad* yanaibua dhamira zipi?

## 1.5 Umuhimi wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu tatu:

Kwanza, utafiti huu utatoa mchango katika taaluma ya fasihi kinadharia na vitendo. Kwa kueleza na kuchambua fasihi simulizi iliyomo katika kitabu cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, tutaweza kuona ni jinsi gani msanii huyu alivyotumia mbinu za fasihi ndani ya kazi zake; *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad.*

Pili, utaongeza maarifa katika nadharia na mbinu za utunzi wa riwaya hususani riwaya za Kiswahili. Aidha, utafiti huu utaweza kutumika katika taaluma ya fasihi, hususani

riwaya. Hivyo, utafiti huu utatumika kama marejeo na kwa maana hiyo, utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo kuhusu riwaya za Kiswahili na riwaya kwa ujumla wake.

Vile vile, utafiti huu utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kutupia jicho katika riwaya za Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu utawapa changamoto watafiti wengine waweze kuchunguza na kuchumbua ufasihi simulizi katika kazi zingine za fasihi ili kuona jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vinatumika katika kujenga tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili.
Tatu, utafiti huu ni malighafi, kwani utatoa mchango mkubwa katika historia ya riwaya na fasihi chambuzi kwa ujumla na vile vile utatajirisha maktaba ya chuo.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchambua ufasihi simulizi katika riwaya za Kiswahili. Pamoja na kuwawapo waandishi na watunzi wengi wa riwaya kwa hivyo utafiti huu, kuwa haikuwa rahisi kuchunguza riwaya za waandishi wote, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kuchambua ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert tu. Sababu ya kumchagua Shaaban Robert ni kwa sababu ni mtunzi mwenye athari kubwa katika fsihi ya Kiswahili. Shaaban Robert ana riwaya nyingi lakini utafiti huu uliamua kuteua zake mbili yaani riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad*. Hii ni kwa sababu isengekuwa rahisi kuchunguza riwaya zote alizotunga Shaaban Robert.

Hivyo utafiti huu ulichunguza na kuchambua kazi mbili tu Shaaban Robert. Kwa maana hiyo kazi zake nyengine za kifasihi hazitoshughulikiwa isipokuwa riwaya zilizotajwa. Kazi za Shaaban Robert na zile za wasanii wengine ambazo hazikushughulikiwa katika utafiti huu, bali ziliweza kurejelewa hapa na pale kwa lengo la kuchunguza na kuchambua vipengele mbali mbali vya fasihi vilivyomo katika kazi hizo.

## 1.7 Hitimisho

Sura hii imeajadili kuhusu usuli wa utafiti, vile vile limejadiliwa tatizo la utafiti. Aidha sura imezungumzia kuihusu malengo ya utafiti, pamoja na kuzungumzia lengo kuu la utafiti. Sura hii vile vile imezungumzia  malengo mahsusi yaliyomo katika utafiti huu, na pia yamejadiliwa maswali ya utafiti. Aidha katika utafiti huu imejadiliwa kuhusu umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka inayohusu utafiti. Sura inayofuata inahusu nini?

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO TANGULIZI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni mapitio ya tafiti za riwaya na fasihi simulizi na sehemu ya pili ni kiunzi cha nadharia.

## 2.1 Dhana ya Fasihi Simulizi na Nafasi yake katika Fasihi Andishi

Wataalamu kadhaa wamewahi kuielezea dhana ya fasihi simulizi. Mathalan, Sengo (1978), Mulokozi (1996), Matteru (1983), Kenguru (2013), Sengo na Kiango (1977), huku wakiwa na mitazamo iliyokaribiana au kutafautiana juu ya dhana hii ya fasihi simulizi. Kwa mfano, Ndungo na Wafula (1993), wanaeleza kuwa, fasihi simulizi ni kongwe, fasihi andishi ilikuja wakati wa uvamizi wa wageni wa Kiarabu na Wazungu na pia Shaaban Robert na James Mbotela ndio waandishi wa kwanza wa hadithi ndefu za Kiswahili katika Upwa wa Afrika Mashariki.

Maelezo hayo tunakubaliana nayo kwani tunaamini kuwa dhana ya fasihi andishi ililetwa na wageni, kwa jina la "Literature," wakiwa na maana ya "uandishi" au "herufi," bila kuzingatia vielezea vya fasihi ya Kiafrika, katika upwa huu wa Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla. Hivyo, dhana hii ya fasihi andishi haikuwapo hadi palipoanza maandishi.

Mulokozi (1996), anaeleza kuwa, fasihi simulizi ni taasisi inayofungamana na muktadha fulani wa kijamii na kutawaliwa na muingiliano wa mambo kama vile, fanani, hadhira,

fani, tukio, pahala na wakati. Na huweza kuwekwa katika kumbo za semi, mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi na ngomezi. Maelezo yanayofafanua sifa bainifu za fasihi simulizi ni muhimu sana katika utafiti wetu huu. Hiii ni kwasababu, Mulokozi amegusia vipengele muhimu ambavyo vitatuongoza katika kufanya uchunguzi wetu wa vipengele hivyo vya fasihi simulizi ndani ya riwaya hizo teule.

Taassisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) (1985) inaeleza kuwa fasihi hujishughulisha na taratibu za jumuiya. Fasihi ni kazi ya sanaa inayochukua jukumu la kutudhihirishia na pengine kututatulia hali zetu za kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Kwa ujumla fasihi ni mdhihirisho ama kioo cha maisha ya jamii na uhusiano wao katika muktadha wa mazingira na maumbile yao. Hivyo ni kwamba fasihi inatunza na kutumbuiza. Maelezo haya yanamaanisha kwamba maendeleo ya fasihi hayana budi kuzingatiwa kuambatana kwa mujibu wa maendeleo ya Jumuiya yenyewe na utamaduni wake. Maelezo haya yalimsaidia mtafiti kuona na kuweza kuchambua kwamba ufasihi simulizi uliomo kwenye vitabu teule vilivyojadiliwa na utafiti huu. Hii inaonyesha kwamba ugunduzi wa maandishi hauna budi kuchota tajriba ya masimulizi ya jamii husika kimaelezo, kimtindo na kimuundo.

Mwai na Ndungo (1991), wamekubaliana kwamba waandishi wengi wa fasihi andishi wameathiriwa na fasihi simulizi, kwa njia moja au nyengine, kuna wale ambao wameathiriwa kifani na kuna wale ambao wameathiriwa kimaudhui au kwa njia zote mbili. Kifani kuna wale ambao wanatumia wahusika kama mazimwi, majini au usimuliaji wa hadithi wa moja kwa moja. Kwa mfano Kezilahabi (1976) katika *Gamba la Nyoka* ametumia mtindo huo. Wengine wanatumia mtindo wa paukwa pakawa au

vitendawili kama inavyofanyika katika fasihi simulizi. Mfano Hussein (1976), katika *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* zimechota mitindo ya fasihi simulizi. Kimaudhui kuna uwiyano mkubwa kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Dhamira nyingi wanazozijidali waandishi wa leo zilikwisha jadiliwa zamani katika fasihi simulizi, kama mapenzi, harakati za kikabila, uchawi na kadhalika. Wanaendelea kusema fasihi andishi haijagundua dhamira mapya kabisa ambayo haijitokezi katika fasihi simulizi.

Mulokozi (1996), anasema kuwa fasihi andishi hutegemea maandishi, ni wazi kuwa fasihi andishi ni changa zaidi kwa vile haikuwepo kabla ya kugunduliwa kwa maandishi. Isitoshe, ilianza kwa kukopa mbinu kutoka katika fasihi simulizi, na mpaka leo bado inaathiriwa na fasihi simulizi. Kadhalika fasihi simulizi kwa kiasi fulani, huathiriwa na fasihi andishi. Kwa mfano baadhi ya hadithi au misemo ya waandishi mashuhuri hutokea kupendwa sana na watu hadi kuingia katika mkondo wa fasihi simulizi ya watu hao. Kadhalika mfano Biblia na Misahafu ni miongoni mwa fasihi andishi ambayo imekuwa na athari kubwa kwenye fasihi simulizi ya mataifa mengine.

Nkwera (1979) anasema Fasihi ni moja, lakini kutoka na jinsi taarifa zilizohifadhiwa na kuathiriwa katika jamii huonekana kuwa kuna fasihi simulizi; mapokeo ya mdomo, na fasihi andishi; habari za kubuni zilizoandikwa, baadhi ya habari hizo zikiwa zinatokana na fasihi simuizi. Nkwera anaendelea kusema kuwa jamii na utamaduni wake, watu na amali zao (ni mambo yanayoathiriwa na kuhifadhiwa na jamii, dini, mila, ujuzi, siasa, sanaa ya jadi na lugha). Kuingiliana kwa utamaduni wa jadi na ukoloni au athari nyengine (nguvu na ushawishi). Husababisha matatizo na migogoro pia maendeleo

duni ya jamii yaletwayo na uchumi, aidha mtindo mzima wa uzalishaji mali na jinsi mali inavyogawanywa.

Hali ya kisiasa, utamaduni wa kigeni na ushirikina. Vile vile harakati za kikabila, yaani msuguano, mvutano na maingiliano katika jamii na matokeo yake ni zalio la athari za jamii na amali zake. Pia majibu na mawaidha ya mwandishi kuhusu kukabili matatizo hayo, ili kuleta na kudumisha furaha na maendeleo ya jamii na pia watu binafsi. Hivyo mazingira na fikra zilizotawala wakati wa mwandishi na ambazo zinamwathiri, Kama vile harakati za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Maelezo ya Nkwera yanaonyesha kuwa fasihi andishi ni lazima kuchota na kuibua mbinu za fasihi simulizi katika kuonyesha uzuri na ubaya ambao unafanywa katika jamii husika. Hali hii ilimsaidia mtafiti kwa urahsi kuweza kuibua na kuelezea ni kwa jinsi gani mwandishi hutumia ufasihi simulizi uliomo katika fashi andishi kulingana na vitabu teule vya Shaaban Robert: *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Naye Kihore (1996), anaona kuwa fasihi andishi na fasihi simulizi ni kazi moja tu. Kwani kazi hizo huweza kutoka katika hali moja na kwenda hali nyengine. Mathalani, fasihi andishi huwasilishwa kwa maandishi na fasihi simulizi huwasilishwa kwa masimulizi. Hivyo, utata huzuka kwa hoja kwamba ziko kazi zilizosimuliwa baadaye, zikaandikwa, na ziko zilizoandikwa baadaye, zikasimuliwa. Mawazo hayo ya Kihore ni kuntu kwa kusema kuwa, hiyo inayosemwa ni fasihi simulizi na hiyo iliyoandikwa ni fasihi andishi zina maingiliano makubwa kwani tofauti yake hujitokeza kwa namna zinavyowasilishwa na kuhifadhiwa.

Kwa upande mwengine TUMI (1988), wana mawazo tofauti na Kihore, wao wanasema kuwa, kazi ya fasihi simulizi, hata ikiandikwa haibadiliki hadhi, huwa imehifadhiwa tu kwa njia hiyo. Maelezo hayo ya TUMI yana mchango mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu. Mtafiti atachunguza tanzu za fasihi simulizi zinazohusishwa katika fasihi simulizi, kama zinavyojidhihirisha katika riwaya ya za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

TUKI (1988:116) inaeleza kuwa fasihi andishi ina misingi yake katika maandishi. Kwa hiyo uzuri wa kazi ya mtunzi utategemea kwa kiasi kikubwa historia. Kihistoria binaadamu alipitia hatua nyingi na ngumu katika maendeleo yake katika enzi za ujima na unokoa maelekezo ya utawala yaliendeshwa kwa maelezo ya mdomo. Kadri maendeleo yalivyojitokeza watu waligundua mambo mengi, pamoja na maandishi. Hapo awali maandishi yalinakili masimulizi, yaani fasihi simulizi iliyohifadhiwa katika maandishi. Maelezo haya yalimsaidia mtafiti kwa kiasi kikubwa, kwa sababu yanaeleza nadharia inayosema chanzo cha fasihi ni jamii yenyewe na mambo yake katika harakati za kila siku. Vile vile yalithibitisha kuwa bila ya vipengele vya fasihi simulizi basi fasihi andishi haina uhai. Hali hii ilimsaidia mtafiti kufafanua vipengele vya fasihi simulizi na jinsi vilivyotumika katika kuibu dhamira, vilivyojitikeza katika kazi teule; *Adlii na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, vilivyotungwa na Shaaban Robert.

TAKILUKI (1981:32) wanaeleza kuwa waandishi hutegemea zaidi habari wanayoipata katika mazungumzo na pia katika vitabu wanavyovisoma juu ya watu mbali mbali. Waandishi wa riwaya za aina yoyote wanaweza kutegemea habari za namna hii katika kubuni wahusika wao. Waandishi wa riwaya ambazo zinaelezea watu wa kale na

vitendo vyao wategemee kabisa habari zinazopatikana katika vitabu vya historia, na vitabu vinavyoelezea maisha ya watu wa kale. Tunapoangalia muhusika wa kitabu cha Mohmed Suleiman Abdalla, anawaelezea wahusika kama walivyo tu pasi na kuonesha dharau au mapenzi. Mfano ni Mwana wa Ging’ingi katika kitabu kiitwacho *Kisima cha King’ingi* labda Mwatenga katika *Siri ya Sufuri*.

Katika riwaya inawezekana pia kukutana na muhusika ambaye sifa au ila zake zimepita mipaka ya kawaida. Wahusika kama hawa huwa kama karagosi au vichekesho badala ya kuonekana kama ni watu wanaolingana na watu wa kweli ndani ya jamii, Mfano muhusika Melikizadeki katika kitabu cha riwaya *Siri za Maisha* kilichotungwa na Emmanueli Mbogo. Hali hii ilimsaidia mtafiti kubaini kuwa hata wahusika wanaobuniwa ndani ya kazi ya fasihi andishi ni wale ambao wanatoka katika fasihi simulizi na pia ilimsaidia kuchunguza vipengele vyengine vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya kazi za Shaban Robert, *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

Matteru (1983:31), anaeleza kuwa fasihi simulizi ndiyo data ya fasihi andishi. Fasihi andishi hutumia fasihi simulizi kuunda maudhui ya maandishi yake. Fasihi simulizi huweza kuwa ni msingi mzuri wa kutoa data itakayotumika kama malighafi ya fasihi andishi. Waandishi wa fasihi ya Kiswahili wananufaika kwa kutumia miundo na fani mbali mbali za fasihi simulizi. Katika kufafanua dhana hiyo, Matteru anawatumia waandishi kama; Shaaban Robert, akitaja vitabu vya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, kuwa mwandishi ametumia miundo ya kiasili.

Kenguru (2013), anaeleza kuwa tanzu za mwanzo kabisa katika jamii zote ni zile zinazohusiana moja kwa moja na fasihi simulizi, kama vile, mashairi, ngano,

vitendawili, visaasili, uigizaji na kadhalika. Kenguru anaeleza kuwa, baadaye tanzu hizi zilijitokeza katika hadithi za maandishi. Maelezo haya ya Kenguru yalimsaidia mtafiti kuchunguza namna tanzu za fasihi simulizi zilizotajwa na zilivyojitokeza katika kazi teule zinazotafitiwa; *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

Mtafiti mwengine aliyewahi kufanya uchunguzi wa fasihi simulizi ni Zaja (1986), aliyenukuliwa na Kenguru (2013), akieleza kuwa, ngano za awali nyingi zilikuwa na wahusika binaadamu na wanyama. Sababu kuu ni kuwa fasihi simulizi ilikuwa njia ya kuelewa na kutawala mazingira au matukio ya mara kwa mara, waandishi wa kazi za kubuni walichukuwa malighafi yao kutoka katika mazingira yao. Maelezo haya ya Zaja yalimpatia mtafiti muelekeo mzuri wa kuchunguza ufasihi simulizi uliomo katika fasihi iliyoandikwa. Ingawa Zaja aligusia vipengele vichache tu, yaani wahusika, mandhari na maudhui, ni dhahiri kuwa, mtafiti alichunguza wahusika na mandhari ya kifasihi simulizi ili kutambua namna yanavyodhihirika katika riwaya teule za Shaaba Robert; *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* zilizofanyiwa uchunguzi.

Maelezo hayo yana umuhimu mkubwa kwani, pamoja na kwamba fasihi simulizi hutumiwa na waandishi wa kazi za fasihi andishi katika ujenzi wa kazi zao, pia vipengele hivyo ndivyo vinavyotumika kufikisha dhamira za mwandishi. Kwa hivyo, katika utafiti huu vilichunguzwa namna vipengele hivyo vilivyotumiwa na muandishi kufikisha dhamira kwa jamii.

### 2.1.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi

Kwa vile kazi hii imenuia kuchunguza vipengele vya Fasihi Simulizi vilivyojitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Hivyo, ni vyema kabla

ya kufanya uchambuzi wa uchunguzi, kwanza, vielezwe vipengele hivyo vya fasihi simulizi. Wataalamu kama vile Mulokozi (1996), TAKILUKI (1981), Balisidya (1987), TUKI (1988), Nkwera (1979), wamejaribu kueleza vipengele ambavyo huwa vinahusishwa na fasihi simulizi.

Mulokozi (1996), amejaribu kugawa vipengele vya fasihi simulizi katika kumbo na kila kumbo ina vipengele vidogo vidogo, ni semi, mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi nyimbo, ushairi maghani na ngomezi

#### 2.1.1.1 Semi

Semi ni tungo au kauli fupi fupi za kisanii zenye kubeba maana au mafunzo muhimu ya kijamii. Kumbo hii hutunza, kama vile; methali, vitendawili, mafumbo na misimu.

#### 2.1.1.2 Mazungumzo

Mulokozi (ameshatajwa) anaeleza kuwa, mazungumzo ni maongezi, katika lugha ya kawaida, juu ya jambo lolote lile. Hata hivyo si kila mazungumzo ni fasihi. Ili mazungumzo yaitwe fasihi lazima yawe na usanii wa aina fulani, yanayomithilisha uhalisia badala ya kuunakili. Hali hii hujidhihirisha katika lugha, katika muundo na mtiririko wa mazungumzo yenyewe na katika namna yanavyotolewa. Mifano ya tanzu zinazoingia hapa ni; hotuba, malumbano ya watani, mizaha na sala.

#### 2.1.1.3 Masimulizi

Masimulizi ni taaluma yenye kusimulia habari fulani yakiwa na usanii ndani yake. Hivyo, hii taalimu ya kisimulizi na fani zake huwa na sifa kama vile; kueleza matukio

kwa mpangilio fulani mahususi, huwa na wahusika yaani watendaji au watendwaji, katika matukio yanayosimuliwa. Aidha hutumia lugha ya kimaelezo. Lugha hiyo wakati mwengine huchanganywa na mazungumzo. Vile vile utambaji au utoaji wake huweza kuambatana na vitendo au ishara. Pia huwa na maelezo ya kweli au ya kubuni na yenye funzo fulani kwa jamii. Masimulizi yana tanzu nyingi. Hata hivyo Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, tanzu zinazofahamika zaidi ni kama vile; hadithi za kubuni ambazo hujumuisha ngano, istiara, michapo na hekaya.

#### 2.1.1.3 Maigizo

Pia, Mulokozi (1996), anaeleza utanzu mwengine wa fasihi simulizi ni utanzu wa umithilishaji. Anaeleza kuwa, umithilishaji unatumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe. Mara nyingi natiki za Kiafrika ni kma vile; ngoma, utambaji wa hadithi, nyimbo na matendo ya kimila, kwa mfano, jando na unyago. Yapo pia matukio yanayoambatana na michezo ya watoto, matanga, uwindaji, kilimo. Natiki nyingi hutumia mapambo maalumu.

#### 2.1.1.4 Ushairi Simulizi

Mulokozi (1996), anaeleza kuwa ushairi simulizi wenye kufuata kanuni fulani za urari wa sauti, mapigo ya lugha, na mpangilio wa vipashio vya lugha. Lugha ya ushairi katika fasihi simulizi hupambanuliwa na lugha ya kawaida kwa namna inavyopangiliwa na namna inavyoingiliana na muktadha wa utendaji. Mulokozi anaendelea kusema kuwa, tanzu za ushairi simulizi ni nyimbo na tenzi.

Katika kufafanuwa kipengele cha wimbo Mulokozi (ameshatajwa) anasema kuwa, wimbo ni kila kinachoimbwa. Hii ni dhana pana ambayo hujumuisha tanzu nyingi. Hata baadhi ya tanzu za kinathari, kama vile hadithi zinaweza kuingia katika kumbo ya wimbo pindi zinapoimbwa. Aina kuu za nyimbo hapa Afrika Mashariki ni tumbuizo; nyimbo za kuliwaza, bembea; nyimbo za kubembeleza watoto, nyimbo za kilimo au maombolezi, nyimbo za jando na unyago, nyimbo za siasa; hizi ni nyimbo zinazoimbwa kwenye shughuli za kisiasa, nyimbo za kuaga mwaka au kuadhimisha mwezi muandamo. Pia kuna nyimbo za dini; hizo huweza kuwa nyimbo za Waislamu, Wakiristo na hata ibada za kijadi.

Aidha tanzu vyengine za nyimbo ni kama vile; nyimbo za taifa; hizi ni nyimbo za kusifia taifa au kabila, Chapuzo; hizi ni nyimbo za kuhamasisha shughuli fulani kama vile kilimo, uvuvi, kutwanga na kadhalika. Pia kuna nyimbo za kazi. Hapa tunapata nyimbo kama vile kimai; nyimbo zihusuzo shughuli za bahari, nyimbo za vita; hizi ni zile ziimbwazo na askari wakati wa vita. Pia kuna nyimbo za watoto; nyimbo hizi ni zile ziimbwazo na watoto wakati wa michezo yao. Vile vile kuna tenzi au tendi: hizi ni nyimbo refu zinazosimulia jambo fulani. Zile zinazosimulia visa vya mashujaa huitwa tendi.

Vile vile katika kufafanua kipengele cha maghani Mulokozi (ameshatajwa) anaeleza kuwa maghani ni ushairi unaoghaniwa au kutambwa hadharani. Mara nyingi sauti ya maghani huwa kati ya uzungumzaji na uimbaji. Aghalabu maghani hutambwa hadharani pamoja na ala ya muziki au bila ala. Baadhi ya ghani huwa refu sana zenye kusimulia

hadithi au historia. Ghani za aina hiyo huweza kuwa tendi-simulizi, sifo, visaasili nakadhalika. Kimaudhui maghani hayana tofauti na nyimbo.

### 2.1.1.5 Ngomezi

Mulokozi (1996), anaeleza ngomezi kuwa ni namna ya kupeleka ujumbe kwa kutumia ngoma, midundo fulani ya ngoma huwakilisha kauli fulani katika lugha ya jamii husika. Mara nyingi kauli hizo ni za kishairi au kimafumbo. Huimbwa wakati wa dharura, aghalabu hutangazwa vita kwa kutumia Ngomezi katika kabila fulani kwa kutumia ngoma.

Balisidya (Matteru) (1987) anagawanya fasihi simulizi katika tanzu tatu ambazo ni nathari, ushairi na semi. Katika kila utanzu kuna vipera vyake ambavyo navyo vina vijipera pia vidogo vidogo ndani yake, uanishaji wake ni nathari, nudhumu na ushairi. Amegawa vipengele hivi kwa upande wa nathari, kuna ngano ambayo ndani yake ina istiara, hekaya na kharafa. Katika tarihi kuna kumbukumbu, shajara, hadithi, historia na epik. Na kwa upande wa visaasili kuna kumbukumbu, tenzi. Kwa nini na kwa maana gani? Kundi la pili la ushairi lina nyimbo ambayo nyimbo imejumuisha bembea, tumbuizo, ngoma, kwaya na miviga. Kwa upande wa maghani kuna majigambo, shajara, vijaghani na tenzi.

Katika uainishaji wake huu baadhi ya tanzu hazionekani, ama tunaweza kusema zimeondolewa kabisa. Mfano visakale na ngomezi. Aidha, Balisidya (ameshatajwa) anaweka utenzi kuwa ni kipera cha visaasili katika kundi la nathari. Hapa anaibua mjadala, kwani kama tujuavyo kuwa utenzi katika fasihi simulizi huhusisha uimbaji

kwa hivyo swali la kujiuliza ni utenzi au ni nathari. Vile vile kuna kuingiliana kwa tanzu, Mfano kumbukumbu na kwanini na kwa namna gani ni tanzu ambazo zinajitokeza katika kundi zaidi ya moja.

TUKI (1988), wanasema ugawaji wa tanzu na fani ya fasihi simulizi si wa moja kwa moja. Hii ni kwasababu ya utendaji na uwasilishaji wake, ni vigumu tanzu hizo kubakia katika hali moja. Tanzu na fani ya fasihi simulizi huingiliana. Wimbo huweza kuwa hadithi na hadithi kuwa methali, msemo na kuwa kitendawili. Tunaweza kugawa tanzu na vipera vya fasihi simulizi kwa kugawanya kutokana na kusadifu matumizi. Kulingana na aina ya lugha iliyotumiwa kuziwasilisha mwanzo wa kuumbwa lugha ya tanzu hiyo.

Kwa hivyo, tanzu na fani ya zote zitaingia katika mafungu matatu ya awali, kulingana na aina ya lugha ya uwasilishaji katika fashi simulizi, na kupata nathari, semi na ushairi. Tanzu hizi zote za fasihi simulizi zimegawika katika makundi mawili nudhumu na nathari. Nathari hujumuisha tanzu na vipera ambavyo ni hadithi, ngano, tarihi, visakale, vigano na masimulizi ya utani. Nudhumu nayo hujumuisha ushairi, nyimbo na maghani.

TUKI (1988), wamegawa fasihi simulizi katika tanzu tatu na pia kila utanzu una aina nyengine ya vipera vidogo vidogo, kuna hadithi ambayo ina ngano, tarihi, visaasili, vigano na soga. Ushairi au nudhumu una ngonjera, maghani, nyimbo na ushairi. Vile vile kundi la semi lina vipera vya misemo, misimu, mafumbo, methali, nahau, vitendawili na mizungu. Kama inavyoonekana katika tanzu hizi tatu, kuna aina nyengine mbali mbali ambapo kila kipera kimoja chaweza kuwa ni mkusanyo wa vipera

mbali mbali vyenye wasifu wa aina moja wa muundo na mbinu za uundaji na namna ya uwasilishaji katika masimulizi. Hivyo basi, mawazo haya yanahitaji kuchunguzwa kwa kina jinsi ya ugawaji wa tanzu za fasihi. Tunahitajika kuangalia wakati pamoja na kuangalia muingiliano wa tanzu. Muingiliano huu hufanya baadhi ya jamii kuwa na jina moja tu kwa fani zaidi ya moja, au majina zaidi ya moja kwa fani ile ile moja.

Nkwera (1979), amegawa fasihi simulizi katika makundi matatu, anaona kuwa kunamakundi matatu ya kazi ya fasihi, anaona kuwa kuna habari za kweli na za kubuni katika fasihi huitwa kazi bunilizi. Kazi zenyewe ni hadithi, ushairi na michezo ya kuigiza. Anaendela kusema kuwa hadithi zimegawika katika visa, ngano na hekaya. Ushairi ni mashairi, tenzi na nyimbo. Katika michezo ya kuigiza ni futuhi, tanzia, yuga na rasma.

Nkwera (kashatajwa), anasema futuhi ni mchezo wa furaha au ushindi wa kitu kilichokuwa kimawaniwa, na watu au makundi ya watu tofauti. Tanzia ni mchezo ya kuhuzunisha au kupatwa na janga. Hivyo michezo hii huchezwa kuonesha huzuni juu ya jambo fulani. Yuga ni michezo inayoonyesha furaha na pia huzuni. Ramsa ni michezo inayochezwa kwa namna ya kukejeliana miongoni mwa watu na vile vile kufanyiana mizaha mbali mbali, kulingana na jamii.

Kutokana na maelezo hayo, yameweza kumsaidia mtafifi kupata uwelewa juu ya uchambuzi wa tanzu za fasihi simulizi na kumsaidia katika kukamilisha malengo yake ya utafifi. Hali hii imeweza kumfanya mtafiti kukamilisha kazi yake kwa usahihi. Vile

vile maelezo hayo yalimsaidia katika kuelewa aina mbali mbali za tanzu za fasihi simulizi.

Mawazo haya ya Mulokozi, TUMI, TUKI, Nkwera na Balisidya yalitusaidia sana katika kufanya utafiti na kusukuma mbele uchunguzi wa vipengele vya fasihi simulizi katika kazi hizi teule. Hii ni kwa sababu vipengele alivyovieleza Mulokozi ndio vilivyotuongoza katika kufanya utafiti wetu, na pia vilikuwa ni muhimili wa utafiti, ambavyo viliongoza namna ya kuvichunguza vipengele hivyo, ili kuona namna vilivyotumika katika riwaya hizo za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siiti Binti Saad.* Jadweli na 1 linaonesha vipengele vya fasihi simulizi kulingana na wataalamu, ambavyo vitachaguliwa vile vitakavyojitokeza kulingana na malengo ya utafiti na ndivyo vitakavyoongoza utafiti huu.

**Jadweli na 1: Vipengele vya Fasihi Simulizi**

| **Namba** | **Vipengele Vya Fasihi Simulizi** |
|---|---|
| 1. | SEMI - methali, vitendawili, simo, lakabu, kauli tauria |
| 2. | MAZUNGUMZO - malumbano wa kijamii, hotuba, sala |
| 3. | MASIMULIZI - muundo, lahaja, hekaya, kisa kale, kumbukumbu, istiara, hadithi, ngano, maigizo ya kidini, mandhari pamoja na dhamira |
| 4. | MAIGIZO - kutegemea shabaha ya miktadha. |
| 5. | NGOMEZI - Kutoa taarifa kwa kutumia ngoma kwa nyimbo |
| 6. | USHAIRI NYIMBO NA USHAIRI MAGHANI - Nyimbo za aina yoyote |
| 7. | WAHUSIKA - wanyama, miti, majabali, miungu, mashetani, mazimwi n.k |
| 8. | DHAMIRA – kujitolea, ushujaa, ukarimu, elimu, ubinafsi n.k |

Chanzo cha data: Mulokozi (1996)

## 2.2 Tafiti kuhusu Riwaya ya Kiswahili

Utafiti aina mbalimbali umefanywa ambao unahusu riwaya za Kiswahili lakini utafiti huo umejikita katika kutoa maana ya riwaya, na uchambuzi wa riwaya, kuchambua vipengele vya fani na maudhui kwa ujumla na pia baadhi ya vipengele vya fani na

maudhui na si katika kuchunguza ufasihi simulizi uliomo katika riwaya. Maana ya riwaya imelezwa na wataalamu wengi, baadhi yao ni kama wafuatao;

Hatuwezi kupata maana ya riwaya kwa kipimo cha ubainishaji wa urefu au wingi wa maneno kwa ukamilifu wa maana ya riwaya. Iwapo tutakubalina na Mphalale (1976) ili iwe riwaya ni lazima maneno 75,000 basi tutakuwa tunaungana kwamba hatuna riwaya katika fasihi ya Kiswahili. Chuachua (2011) anafasili kuwa riwaya ni kazi ya kubuni ya kinathari yenye uchangamani wa fikra, msuko, mandhari na uhusika unaosawiri binaadamu na maisha yake. Hii inaonyesha kwamba tunapozungumzia uchangamani, ni ile hali ya kuunda kazi kisanii kwa kutumia mbinu mbali mbali za kiubunifu (kiumbilizi), na ndipo unamfanya kumfikirisha msomaji na uchangamani ndio kigezo kikuuu kinachotofautisha riwaya na aina nyengine za nathari.

Maelezo yaliyotangulia, yanakubalika kwa maoni yetu kwasababu yanaonyesha vigezo vilivyokusanya maana ya dhana ya riwaya kwa mkusanyiko mkubwa wa wataalamu wengi kuonyesha vigezo vya urefu, uhusika wa kina, uchangamano wa mtindo na uzito wa kidhamira, masimulizi kwa kugusa nyanja mbali mbali za maisha zinazohusu walimwengu na vitu vinavyowahusu, mawanada ya hadithi, suala la wakati na matumizi ya mandhari. Hatumaanishi ya kuwa ni lazima pawepo aina zote za vigezo vilivyotajwa lakini pawepo na asilimia ya kutosha (kubwa) kuikamilisha kazi hiyo. Tunakubaliana ya kuwa vigezo hivyo vitakamilisha kuijua dhana ya riwaya na kuitofautisha na aina nyengine ya nathari. Kitu kitachotuwezesha kusema kwa mawanda mapana kuwa vitabu vya Shaabani Robert cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* ni miongoni mwa riwaya.

Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kuwa kuzuka miji na viwanda kulistawisha uandikaji wa riwaya na usomaji kupanuka. Maendeleo katika vipengele vyote vya maisha, kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii, yalizusha haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ambao uchangamano wake wa kifani na kimaudhui ungedhibiti nyanja hizi zote.
Aidha mabadiliko hayo yalileta matabaka, ambapo palizuka tabaka jipya la mwabwanyenye, walihodhi viwanda na nyenzo nyingine za kiuchumi. Hivyo tabaka hili lilitaka fani mpya katika fasihi kwa sababu ya kipato cha fedha za kununulia vitabu na magazeti, na kupata wakati wa ziada wa kujisomea.

Fani hiyo ya riwaya ilitawaliwa na ubinafsi. Ubinafsi huu ulijidhihirisha kiitikadi, mfano riwaya ya Robinson Cruisoe (1719), hudhaniwa kuwa ni riwaya iliyosawiri mawazo ya juu ya kibepari, kwa kumtumia muhusika Friday ambaye alionekana bado kustaarabika. Vile vile ubinafsi ulionekana katika kanuni za utungaji wake kwa kuepukana na kanuni za jadi.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa mageuzi ya kijamii na kisiasa pia yalifungamana na mabadiliko ya kiuchumi tuliyoyataja. Mataifa ya Ulaya yalianza kujitegemea kwa kuepukana na Dola iliyokuwa tukufu ya Kirumi. Hivyo Mataifa ya Ulaya yalianza kujipambanua kiutamadauni na kisiasa pia walijenga utamaduni wao kitaifa na mifumo ya elimu. Vile vile walianza kutumia mfumo wao wa maandishi katika lugha yao. Hata misahafu ya dini, kama vile Biblia ilianza kufasiriwa kwa lugha ya Kidachi mwaka elfu moja mia tano na thalathini na nne (1534), kila elimu ilipotanuka na ndipo watunzi walipoengezeka na hivyo kuwa hadhira nzuri ya watunzi wa riwaya.

Mulokozi (1996) anafafanua kuwa ugunduzi wa teknolojia ya upigaji chapa vitabu kwa kutumia herufi zinazohamishika, mathalani mgunduzi aitwae Gutenberg huko Ujerumani mwaka elfu moja mia nne na hamsini (1450) ulirahisisha kazi ya uchapaji vitabu, Hali iliyopelekea vitabu kuwa bei nafuu na kupatikana kwa wingi.

Ndongo (1991) anaeleza kuwa kuzuka kwa viwanda kuliwafanya waandishi wengi kuandika maandiko yaliyo marefu hali hii ilisababisha kapatikana kwa wasomaji wengi hasa wanawake ambao waliachwa majumbani baada ya waume wao kwenda kufaya kazi viwandani. Kwa kuwa wanawake hasa wale wa tabaka la juu walikuwa na watumwa wa kuwafanyia kazi za nyumbani. Kwa hivyo kuzuka kwa riwaya tunaweza kusema kulifungamana na mfumo wa ubepari.

Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kuwa kuzuka kwa mitambo ya kupigia chapa, viwanda pamoja na miji, hivi vilikuwa vyombo mahsusi vilivyokuza utanzu wa riwaya. Kulikuwa na uwezekano wa kuandika maandiko marefu marefu kwa urahisi kwa kutumia mitambo ya kupigia chapa. Hali iliyofanya nakala nyingi za maandiko hayo zingalitolewa na kusambazzwa kwa rahisi. Miongoni mwa riwaya za mwanzo kuandikwa kwa Kiswahili ni ile riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934), kilichoandikwa na Mbotela (1934), kinaelezea kwa kusimulia habari za watumwa na uhuru wake pamoja na harakati za biashara ya watumwa katika mwambao wa Afrika Mahariki. Kitabu hiki ijapokuwa kimeandika habari za watumwa lakini kina taathira kubwa za kikoloni.

Mashindano yaliyoanzishwa yalikuwa ni chachu ya kuanzishwa kwa riwaya ya Kiswahili. Kutokana na mashindano hayo yaliyoanzishwa na Taasisi, waandishi wengi wa Kiafrika walijitokeza na kuandika riwaya. Mifano ya waandishi hawa ni Shaaban Robert (1960), ambaye vitabu vyake vilichota kwa kiasi kikubwa utamaduni wa wageni, vitabu kama vile *Kusadika* na *Kufikirika*. Ali Jemadar naye aliandika riwaya ya *Nahodha Fikirini*, wengine walioshiriki katika mashindano haya ni Moh’d Saleh Farsy (1960) alitoa kitabu cha *Kurwa na Doto*, Mohmed Suleiman Abdalla (1960), aliandika wa *Watu na Wanawe*.

Katika maendeleo ya riwaya za Kiswahili, uandishi umepiga hatua fulani, hasa baada ya uhuru, nje ya ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki, Mantiki, imeongezeka maradufu. Kwani maudhui, mantiki, mtiririko hata mtindo inasonga mbele kila uchao. Hivyo riwaya nyingi zimeandikwa miaka ya sabiini na thamanini. Waandishi kama vile Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed Mohamed, Suleiman Mohamed, Mohamed Said Abdalla, ndio washika bendera kwa kuzingatia kigezo cha maudhui na uumbaji wa kisanaa.

Tunapochunguza maelezo hayo ni dhahiri kuwa chanzo cha riwaya za Kiswahili ni mchango mkubwa uliotokana na biashara na mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Hali hii ilianza Ulaya na kuja Afrika, kwa kutumia biashara ya baharini. Ambapo biashara hii ilipotokea Ulaya kuja Afrika iliathiri kwa kiasi kikubwa mila, silka na desturi za Waafrika. Hali iliyopelekea kufuata uhalisia wa Kiafrika na kuwa mchanganyiko kati ya Uafrika na Uzungu. Ndipo pakapatikana kitu kiitwacho riwaya inayotokana na fasihi andishi badala ya hadithi inayotokana na fasihi simulizi.

Kwa upande wa uchambuzi wa riwaya, kazi ambazo zimefanyika kuchambua riwaya ni pamoja na Chuachua (2008), Chuachua (2009), Senkoro (1976), Senkoro (1982), Msokile (1993), Sengo (1975), Taib (2008), Tiab (2009) na Mong'eri (2000). Chuachua (2008), alifanya utafiti unaohusu "Taswira katika riwaya za Shaaban Robert", alichunguza athari mbali mbali alizotumia Shaaban Robert katika riwaya zake. Kwa ujumla, kwa kuangalia taswira, hivyo alifanya uchambuzi wa dhamira na kuliacha suala la fani. Hivyo utafiti huu umetuachia pengo ambalo linahitajika kuzibwa.

Chuachua na wenzake (2009), waliandika makala inatoitwa "Shaaban Robert Vita na Ukoloni", walifanya uchambuzi katika vitabu vya Shaaban Robert na kuthibitisha kuwa kazi za Shaaban Robert zimejaa ukoloni. Kwa kuonyesha ni namna gani wakoloni walitesa, kuwakandamiza pamoja na kuwanyonya watu weusi kwa miaka mingi kadhaa. Katika uchambuzi wao, walionyesha vipengele vya dhamira ya kupinga ukoloni na kutafuta ukombozi, kwa kutumia vitabu vya *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1909), *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1949) na *Mwafrika Aimba* (1969). Kazi hizi zote zilijishughulisha na itikadi ya Kisoshalisti tu.

Senkoro (1976), aliandika makala inayoitwa "Utamaduni katika Riwaya za Kiswahii", kwa ujumla aliangalia athari za utamaduni katika riwaya za Kiswahili, pamoja na mambo mengine. Alifafanua kwamba riwaya ya *Adili na Nduguze* ina umbo la ngano na wahusika wake ni majini na mashetani n.k. Pia anaeleza kuwa Shaaban Robert amezikashifu dini za Kiafrika kwa kuwa zina mila za kuabudu mizimu. Maelezo ya Senkoro (1976) yanafaa kujadiliwa kwa kina, kwani aliyoyasema yanaonyesha kuwa,

hakuangalia mila, desturi, silka pamoja na utamaduni wa Afrika, kwa wakati ambao ulikuwa haujapata athari kubwa za wageni walioingia Afrika.

Senkoro (1982), alifanya kazi ya kuchambua kitabu cha *Siku ya Watenzi Wote*, na kuchambua kipengele cha dhamira na alifafanua kwamba, dhamira iliyotawala ni ile ya ujenzi wa jamii mpya itakoyokuwa ya kiutopia. Kwa maoni suala hili linahitajika kuangaliwa kwa jicho la ndani kabisa, kwani mbinu za masuluhisho ya kuweza kujenga jamii aliyoikusudia Shaaban Robert pengine zinatekelezeka. Senkoro (1982), inaonyesha hakuangalia itikadi kwa usahihi ya mwandishi wa kitabu cha *Siku ya Watenzi Wote* na jamii ambayo imeandikiwa kazi hiyo kwa kutazama mila, desturi, silka na utamaduni wa jamii.

Sengo (1975), alifanya uhakiki wa kazi za Shaaban Robert, uhakiki wa Sengo unaweka bayana dhamira zilizotamalaki katika kazi zake. Japo kapigania utu bora, uungwana, ustaarabu, heshima, adabu, njema, haki na kila jema. Maelezo hayo yanaonyesha ujumla jumla, bado yanahitajika kujadiliwa kwa kina kwani hayakuonyesha ni kitu gani au msukumo gani uliomfanya Shaaban Robert kutunga kazi kwa kutumia dhamira hizo. Je? Jamii haina mambo yake wanayofuatwa katika kutengeneza au kufanya jambo fulani kutokana na mila, desturi, silka na utamaduni wake.

Tiab (2008), alifanya uchambuzi wa kazi mbali mbali za Shaabani Robert, ambazo kwa maoni yake Taib, kazi hizi zina maudhui ya Kiislamu na kwamba zinafaa kuhakikiwa na kuchambuliwa kwa makabala wa nadharia ya Uislamu. Anafafanua kwamba hata kazi za Shaaban Robert, hazipaswi kuhakikiwa kwa mikabala ya Kimagharibi kwani mikabala hii ina nafasi kubwa ya kuweza kupotoa maudhui ya kazi zenye maadili ya

dini husika. Maelezo haya yanaweza kujadiliwa kwa ukweli, sio mikabala yote inapotosha Uislamu pale inapoteuliwa kufanyika kwa utafiti. Kutokana na maelezo hayo, inaonyesha kuwa unapochagua mkabala tuhakikishe kuwa utafaa kwa utafiti, mfano mwingilianamatini tunaweza kutumia bila ya kupotosha kazi za Shaaban Robert. Tunapoangalia mkabala wa kimuundo tunaangalia jinsi gani lugha inavyowiyana na maana iliyobeba kutokana na jamii yake. Pia mwingilianomatini tunaangalia kazi moja kutumika ndani ya kazi nyengine kulingana muktadha wa kijamii

Taib (2009), alifanya uchambuzi kuhusu “Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi”, Mtafiti wa maandishi haya anasema msingi wa falsafa ya mwandishi huyu ni udhanifu, na kwamba dini ndio muelekeo wa vielelezo vyake. Mwandishi huyu ameigawa falsafa katika makundi matatu, utu wema, siasa na dini. Taib anaeleza kuwa lengo la Shaaban Robert ni kuelimisha jamii kuhusu uongozi mwema unaofaa na kulaumu dhuluma iletwayo na uongozi unaokandamiza raia. Tunajiuliza suala ni siasa ipi ifuatwe ili kujenga uongozi mzuri. Hapa tunasema tuiyangalie jamii kimuundo katika mamlaka yake katika fikra, mila, desturu, silka na utamaduni.

Mong’eri (2000), alifanya utafiti na kuchambua utetezi wa maadili katika nathari za Shaaban Robert pekee. Anaeleza kwamba tunaweza kugawa maadili katika makundi matatu, kundi la kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lengo la utafiti huu ni kushughulikia suala la itikadi katika riwaya zake, tunaitazama itikadi kama zana ya utekelezaji wa majukumu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## 2.3 Pengo la utafiti

Tunapoyatalii maandiko hayo, tunabaini kuwa hakuna mtafiti aliyeshughulikia moja kwa moja suala la ufasihi simulizi katika ya riwaya za Shaaban Robert. Watafiti na waandishi wachache wamejaribu kulieleza kidogo suala la dhamira na fani, na kuacha vipengele vingine vidodo vidogo vinavyojenga kazi za riwaya teule za Shaaban Robert. Watafiti na waandishi hawa wamechambua dhamira na fani na kuonyesha ujumla wake, bila ya kuonyesha ufasihi simulizi uliomo ndani ya kazi hizo. Hata hivyo fasihi andishi hujengwa na vitu vingi, na pia ina mambo mengi ya kuchunguzwa katika muuundo wa riwaya, kwa kutizama fani ya jamii husika pamoja na historia, mahusiano na muundo wake. Hivyo utafiti huu umeziba pengo hilo kwa kuchunguza ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert, ili kubaini jinsi msanii huyo anavyotumia vipengele vya fasihi simulizi kama malighafi ya utunzi wa riwaya zake.

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Katika utafiti wa kazi ya fasihi, zipo nadharia ambazo zinaweza kutumika kuchunguza na kuchambua kazi ya fasihi. Kila nadharia inaweza kufaa au kutokufaa kuzichambua kazi ya fasihi, Kwa kuzingatia lengo la utafiti unaotaka kufanywa. Katika utafiti tunaweza kutumia nadharia mbali mbali kama vile Ufemenisti, Uumbaji, Mwitiko wa msomaji, Simiotiki au kiujumi, na nadharia ya mwingilianomatini. Hata hivyo kutokana na malengo ya utafiti huu, tuliona kuwa misingi ya nadharia nyingine zisingetufaa katika kubaini ufasihi simulizi katika riwaya. Kwa hiyo tuliona kuwa nadharia ya mwingilianomatini inafaa kwa utafiti wetu. Sehemu ifuatayo inajadili kuhusu nadharia ya mwingilianomatini.

### 2.4.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) na Ndumbaro (2013), wanasema Mwingilianomatini ni moja ya nadharia za fasihi, ambayo hutumika katika kuchunguza, kuchambua data za utafiti na kubaini kazi moja ndani ya kazi nyengine katika kazi za fashi. Wamitila (2002), Njogu na Wafula (2007) na Ndumbaro (2013), hii iliyoasisiwa na mfaransa, Julia Kristeva, alizaliwa 24/06/1941 huko Bulgaria, Kristeva aliizua nadharia hii ya Mwingilianomatini kutokana na fikra zilizotokana na nadharia ya Usemezano ya Mrusi Mikhail Bakhtin (1895 – 1975). Bakhtin, anaamini katika nadharia hiyo ya Usemezano kuwa kazi ya fasihi ina alama ya sauti ambazo huingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizopita, zilizopo kwa sasa au zitakazotungwa baada hizo zilizotangulia. Hii ina maana kuwa athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizopo kwa sasa au zitakazotungwa baada hizo zilizotangulia.

Hivyo mawazo ya Bakhtin yalifanya kuzuka kwa mawazo ya Kristeva, Kristeva aliyaendeleza na kuyatanua mawazo hayo na ndipo ilipozuka nadharia yake ya mwingilianomatini mnamo mwaka 1960. Kristeva katika nadharia yake hiyo anaamini kuwa, katika kazi yoyote inayomuhusu mwanadamu haiwezi kuangaliwa peke yake, hivyo matini hiyo itakuwa na mafungamano na kazi nyengine inayochangiana nayo na kukamilishana katika miktadha mbali mbali. Hii ina maana kuwa katika kazi za kisanaa za fasihi kuna mafungamano ya kuhusiana na kutegemeana, hivyo si rahisi kuchunguza chanzo au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa hali yoyote ile kutakuwa kuna mambo yanayochangiana katika kazi zilizopo au zilizotangulia kubuniwa.

Vile vile nadharia ya mwingilianomatini inashikilia msimamo kwamba, matini kufanana na kuchangizana na kuamini kuwa matini ya kifasihi haiwezi kujitegemea kipekee. Pamoja na hayo mitindo fulani ya kiusemi na misimbo mwingilianomatini huhusisha pia, ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi zitakozotungwa. Hii inamaanisha kuwa nadharia ya mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ile tajriba ya uingiliano wa mitindo ya kitaashira.

Kwa ujumla, mawazo ya Kristeva kuhusu na nadharia ya mwingilianomatini ni jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya kazi kuwa na maana kamili, ambapo dhana ya matini huangaliwa kama ina utegemezi na matini nyengine kwa kuitwa "mwanda wa ki – mwingilianomatini". Hii ina maana, kwa mujibu wa Kristeva, matini yoyote ile huchukua au kujipamba kutokana na kazi nyingine kwa kuzichawanya katika mawanda ya kimwingilianomatini.

Hivyo nadharia hii ilitufaa kwa utafiti wetu kwasababu tulichunguza ufasihi simulizi uliomo ndani ya fasihi andishi, ni sawa na kusema kuwa matini moja imo ndani ya matini nyengine. Kulingana na malengo ya utafiti huu tuliona kwamba nadharia zilizotufaa zaidi ni nadharia ya Mwingilianomatini. Katika utafiti huu tulitumia nadharia ya mwingilianomatini ili kuchunguza na kubainisha matumizi ya mbinu ya fasihi simulizi katika riwaya ya *Adili na Nguguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad*. Ijapokuwa nadharia yoyote yaweza kufaa katika utafiti, lakini sababu ya kuchagua nadharia hii, ni kutokana na kuona kuwa misingi yake ilihusiana sana na malengo ya utafiti wetu. Kwa hiyo tuliona kwamba, kwa kutumia nadharia hii tutaweza kufikia malengo ya utafiti huu kwa kuonyesha uhusiano na kuathiriana kwa kazi za fasihi simulizi katika riwaya

kukamilisha utafiti wetu. Vilevile tuliona kuwa, misingi ya nadharia mwingilianomatini misingi yake itatuongoza katika kuchambua, kubaini na kujadili matumizi ya vipengele vya fasihi katika riwaya teule.

Kwa kutumia nadharia hii, tuliweza kubainisha vipengele vya fasihi simulizi kama vile; nyimbo/ushairi, wahusika, matani, masimulizi, hadithi, methali, semi, mandhari, wahusika na ishara. Nadharia hii pia ilitusaidia kubaini dhamira zilizojiegemeza katika matumizi ya fasihi simulizi katika utunzi wa riwaya.

Hivyo, nadharia ya mwingilianomatini ilitumika kuchunguza na kubaini ufasihi simulizi uliomo katika fasihi andishi kwa kutumia vitabu vya riwaya za Shaaban Robert ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Bint Saad*. Tulichunguza ni jinsi gani fasihi simulizi ilivyoijenga jamii ndani ya fasihi andishi kulingana na mila, silka, desturi na utamaduni wa jamii.

### 2.5 Hitimisho

Sura hii imepitia na kujadili juu ya maaandiko mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi simulizi, tafiti za riwaya ya Kiswahili na hatimaye kuibua pengo la kimaarifa ambalo utafiti huu ulikusudia kuliziba. Katika sura hii imeelezwa kuwa nadharia ambayo imeongoza utafiti. Hivyo basi, sura inayofuata inabainisha kuchambua na kujadili mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya data za utafiti huu.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inajadili juu ya mkabala wa utafiti, mbinu, na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu saba; sehemu ya kwanza inahusu eneo ambalo utafiti ulifanyika, sehemu ya pili ni kundi lengwa, sehemu ya tatu ni sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli, sehemu ya nne ni mbinu za ukusanyaji data, sehemu ya tano inabainisha zana zilizotumika kukusanyia data na sehemu ya sita inajadili juu ya mbinu za uchambuzi wa data wakati sehemu ya mwisho ya sura hii inatoa hitimisho la sura.

### 3.1 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004), ni mwendelezo wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa unajulikana kama mbinu ya uteuzi wa sampuli. Mbinu yenye madhumuni maalumu na dhamira zinahusisha uteuzi wa vitu kama sampuli unaofanywa na mtafiti kwa madhumuni maalumu na dhamira kutegemeana na taarifa zinazohitajika kupatikana kwa ajili ya utafiti.

Kothari (1990) anaeleza kuwa siyo rahisi kukusanya taarifa zote kutoka kwenye kundi zima, yaani kundi lengwa. Na anasema kuwa zipo mbinu mbalimbali za uteuzi wa sampuli. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu tatu, yaani: mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu, uteuzi rahisi wa sampuli na uteuzi bahatishi. Matumizi

ya mbinu hizi, yalitokana na malengo ya utafiti huu kwa kuzingatia nadharia inayoongoza utafiti huu. Utafiti huu ulitumia mkabala wa utafiti usio wa kitakwimu. Hivyo matumizi ya mbinu hizi tatu za uteuzi wa sampuli yana umuhimu mkubwa ili kufikia lengo ya utafiti huu.

**3.2 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyikia katika maeneo ya jiji la Dare-es-salaam (Chuo Kikuu Huria) na Pemba (Zanzibar). Uteuzi wa maeneo haya ya utafiti ulitokana na sababu zifuatazo; kwanza kwa upande wa Dar es salaam ni eneo ambalo kuna maktaba za kutosha, upatikanaji wa vitabu, wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ambao pia wanatarajiwa wataweza kumpatia mtafiti data za kutosha mtunzi wa kazi hizi kwa sababu ya kumbukumbu zao nyingi zimehifadhiwa katika sehemu hizo. Pia kwa kutumia Pemba kama eneo la utafiti, tuliamini kuwa itakuwa rahisi kuwapata wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria wanaosoma fasihi ya Kiswahili. Dar es salaam ni eneo ambalo kuna Maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu Cha Dae-es –salaam. Kwa maana hiyo, ilikuwa rahisi kupata vielelezo vinavyomuhusu Shaaban Robert, kwa kusoma taarifa zake zinazohitajika katika utafiti huu. Vile vile ilikuwa rahisi kuwapata watu ambao waliwahi kusoma kazi zake, kwa kuandika makala au kuzifanyia utafiti. Kwa hiyo tulitegemea kupata data za kutosha. Kwa upande wa Pemba ilikuwa rahisi kupata data za mwandishi wa kitabu cha *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad*, kwasababu vitabu hivi viliwahi kutumiwa mashuleni na bado vinatumika na pia watu wa kawaida wanendelea kuvisoma. Hivyo, Dar es salaam na Pemba ndio maeneo tuliyoyaona kuwa ni muhimu na kufaa kukamilisha utafiti huu.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Katika uteuzi wa sampuli utafiti ulitumia sampuli tatu: uteuzi wa madhumuni maalumu, uteuzi wa nasibu/mbinu bahatishi na mbinu ya uteuzi rahisi, zimejadiliwa kama ifuatavyo :

#### 3.3.1 Kundi Lengwa

Kulingana na (Kothari, 2004; Bryman, 2004; Komba na Tromp, 2006) kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Cooper (1989) na Vans (1990), wanaeleza kuwa kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni walimu na wanafunzi wa umahiri katika fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria hususani Idara ya Fasihi Taaluma za Kiswahili Pemba, wanafunzi wa Sekondari ya Uweleni kidato cha tano (5) na kidato cha sita (6) ambako tuliweza kuwapata wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili. Kwa upande wa walimu, mtafiti aliwateua kulingana na madhumuni maalumu. Hapa mtafiti alizingatia ufahamu na taarifa alizopata kuwa nani ni mwalimu wa fasihi ya Kiswahili hususan riwaya kwa Kiswahili na nani ni mwalimu anayefundisha fasihi kwa jumla.

Kundi lengwa la utafiti huu liliteuliwa kulingana na sifa na umuhimu wa kundi hilo katika utafiti huu; kwanza kwa mwanafunzi lazima awe anasoma au kulifahamu vyema somo la fasihi ya Kiswahili na umuhimu wa kila kundi katika utafiti huu. Kwa mfano, wanafunzi wa umahiri katika fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria waliteuliwa kwa kigezo kuwa ni wanafunzi wanaosoma fasihi, wana maarifa ya nadharia za uchambuzi wa kazi za fasihi na pia wana ujuzi na maarifa katika matumizi ya nadharia

na mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi. Vile vile kigezo cha kuwa wanafunzi hawa wanasoma riwaya kwa Kiswahili kilifanya kundi hili kuwa ni rasilimali ya kutosha katika utoaji wa data za utafiti huu.

Sifa nyingine ya wanafunzi wa umahiri katika fasihi ya Kiswahili wa fasihi Chuo Kikuu Huria ni kwamba walipatikana kwa urahisi. Lakini pia ilikuwa rahisi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria kwa sababu wanasoma darasani na kuna eneo mahsusi la kuweza kuwapata na kuwatambua kuwa hawa ni wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, sababu hizi ndizo zilizomfanya mtafiti kuchagua wanafunzi wa umahiri katika fasihi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu Huria, kuwa wahojiwa wake katika utafiti huu.

Walimu na wahadhiri wa fasihi wa muda mrefu ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wanaofundisha kozi ya fasihi, wana ujuzi na maarifa ya kutosha katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa jumla. Hivyo kwa kutumia kundi hili tuliweza kupata data za kutosha kuhusu Shaaban Robert kutokana na vitabu vyake teule katika utafiti huu.

Kwa upande mwingine, walimu wa fasihi wa muda mrefu ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wanaofundisha kozi ya fasihi, wana ujuzi na maarifa katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa jumla. Vile vile uliwahusisha wazee na vijana wanaoishi nje ya eneo la Mkoani – Pemba, wazee ambao ni kawaida kutamba hadithi kwa vijana na pia vijana ambao hutolewa hadithi za kale, ambao huwa na uzoefu wa kutoa hadithi na wanosimuliwa kuweza kuhifadhi hadithi hizo na kusimulia wenzao, hadithi kama zile za safari,

vichekesho, ujanja na pia za watu mashujaa waliokuwepo Ukanda wa Pwani Afrika Mashariki. Zikiwemo zile ambazo baadae ziliandikwa kama riwaya, mfano *Adili na Nduguze*, *hadithi ya Mkama Ndume*, *Mwana wa Mwana*, *Mwinyi Mkuu, Siti Binti Saad* n.k. Hivyo kwa kutumia kundi hili tuliweza kupata data za kutosha kuhusu vitabu vya *Adili na Nduguze* pamoja na wasifu wa *Siti binti Saad* kwani hadithi zao sio ngeni kwa wasimulizi wa hadithi na wasikiliza hadithi za utamaduni wa watu wa Afrika Mashariki.

### 3.3.2 Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Uteuzi, kwa kigezo cha madhumuni maalumu, ni uteuzi wa kuzingatia sababu mahsusi. Kombo na Tromp (2006) wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti, kwa makusudi, hulenga kuteua kundi la watu ambao anafikiri kuwa ni rasilimali inayotegemewa katika utafiti wake. Kwa hiyo, mbinu hii ni bora na ya muhimu katika utafiti kwa sababu, baadhi ya watu, katika kundi lengwa, walionekana kuwa na uwezo na ni rasilimali kubwa zaidi katika kutoa data za utafiti huu kuliko wengine. Kwa mfano, suala la kiwango cha ufahamu wa fasihi, nadharia na uhakiki kati ya wanafunzi wanaosoma fasihi na wale wasiosoma fasihi, kati ya walimu wanaofundisha fasihi, hususani riwaya. Katika uteuzi wenye madhumuni maalumu uteuzi hufanywa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusu na maswali ya utafiti, kuliko kigezo cha uteuzi nasibu au wa kubahatisha. Hivyo, Katika mbinu hii, wahojiwa waliteuliwa kwa madhumuni maalumu kutokana na nafasi zao kwa kujuwa kuwa wao ndio rasilimali ya jamii juu ya data ya utafiti.

Sababu nyingine iliyomfanya mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba; mtafiti alikuwa na taarifa juu ya kuwapo kwa makundi yenye ujuzi, maarifa na uzoefu katika fasihi kwa Kiswahili na riwaya kwa Kiswahili, makundi hayo ndiyo yaliyokuwa rasilimali ya data

ya utafiti huu. Hivyo basi, mbinu hii ilitumika kufanya uteuzi kutoka kwa walengwa wa utafiti huu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaosoma riwaya kwa Kiswahili waliteuliwa kwa kigezo kuwa wanaelewa nadharia za uchambuzi wa riwaya ya Kiswahili. Wanafunzi walioteuliwa ni wale wenye maarifa ya riwaya kwa Kiswahili, historia na mabadiliko yake na hivyo, wana uwezo wa stadi za uchambuzi wa vipengele vya fasihi simulizi katika kitabu cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Kigezo hiki pia kilitumika kwa walimu wa fasihi waliobobea katika riwaya kwa kuzingatia uzoefu na maarifa na ujuzi juu ya nadharia za uchambuzi na uhakiki wa riwaya.

Kwa jumla, mbinu ya uteuzi kwa madhumuni maalumu, ilimsaidia mtafiti kupata kundi la watu wenye uzoefu, stadi na maarifa katika nadharia na uhakiki wa fasihi na riwaya kwa Kiswahili, na hatimaye, kupata data ambazo ni mhimili wa utafiti huu. Vile vile, data zilizopatikana katika makundi hayo, zilimsaidia mtafiti kupata na kufanya majumuisho mahususi aliyoyakusudiwa kulingana na madhumuni ya utafiti.

### 3.3.3 Uteuzi nasibu/Mbinu bahatishi

Mbinu nyingine ambayo ilitumika katika uteuzi ni mbinu ya uteuzi nasibu. Kombo na Tromp (2006) wanaielezea mbinu hii kuwa, ni mbinu ambayo hutumia watu ambao ni hadhira iliyomilikiwa, yaani watu ambao mtafiti alikutana nao bila kutarajia. Katika mbinu hii, wahojiwa huwa ni wale watu ambao walipita na kuonesha kupendezwa na utafiti unaofanywa. Mbinu hii ilitumika kuwateua wahojiwa ambao ni watoa hadithi na wapenda kusoma vitabu vya fasihi hususan vitabu vya Shaaban Robert. Kwa kuwa siyo rahisi, kuwafahamu watu hao, mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuwashirikisha pale tu mtafiti

alipokutana nao na alipata taarifa kuhusu kitabu cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data na taarifa za kutosha kuhusu hadithi ambazo Shaaban Robert kaziandika na kuwa riwaya.

### 3.3.4 Mbinu ya Uteuzi Rahisi

Mbinu hii ilitumika katika kupata uteuzi wa utafiti huu. Kwa kutumia mbinu hii ya uteuzi rahisi, Mtafiti alichukua orodha ya majina ya wanafunzi wa sekondari, na alitumia nafasi kila baada ya mwanafunzi wa nne, aliteua jina la mwanafunzi ambaye alishiriki katika kutoa data za utafiti. Hivyo, kwa ujumla utafiti huu ulikuwa na jumla ya wahojiwa 64 na mchanganuo wake ni kama inavyojionyesha katika jedwali lifuatalo namba 2:

**Jedwali namba 2 - Idadi ya Washiriki wa Utafiti**

| **Namba** | **Aina** | **Jinsia** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Ke** | **Me** | |
| 1. | Wanafunzi wa umahiri wa Chuo Kikuu wanaosoma riwaya kwa Kiswahili | 09 | 09 | 18 |
| 2. | Wanafunzi wa sekondari (Uweleni) | 15 | 15 | 30 |
| 3. | Wlimu chuo Kikuu Huria | 00 | 02 | 02 |
| 4. | Walimu wa fasihi Sekondari Uweleni | 04 | 04 | 10 |
| 5. | Waliowahi kusoma kazi za Shaaban Robert | 03 | 03 | 06 |
| 6. | Wazee wasimulizi hadithi | 01 | 01 | 02 |
| 7. | Vijana wasikiliza hadithi | 01 | 01 | 02 |
| **JUMLA** | | | | **70** |

**Chanzo kutoka data za Utafiti**

## 3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ni zoezi linalohitaji mbinu muafaka zinazokubalika kutokana utafiti husika. Bila matumizi ya mbinu stahili data stahili za utafiti haziwezi kupatikana.

Hivyo, katika kukusanya data za utafiti huu mbinu mbalimbali za ukusanyaji data zilihusishwa ambazo ni usomaji wa machapisho, majadiliano ya vikundi, usaili na dodoso.

### 3.4.1 Mbinu ya Usomaji wa Machapisho

Mbinu hii ni mbinu kuu iliyotumika kukusanya data za utafiti huu. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kusoma na kuchambua kitabu cha riwaya cha *Adili na Nduguze* na kitabu cha riwaya cha *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Katika kuchambua riwaya hizi, mtafiti alibainisha vipengele vya fasihi simulizi katika vitabu vya Shaaban Robert. Baaada kubainisha vipengele vya fasihi simulizi alipanga katika makundi mahususi, mbinu hii ilitusaidia sana kubaini vipengele hivyo. Pamoja na ubora wake bado ilionekana kuwa kuna haja ya kupata data zaidi kuhusu vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya. Hivyo tuliamua kutumia mbinu ya usaili ili kupata data zaidi.

### 3.4.2. Mbinu ya Usaili

Babbie (1992) anasema kuwa usaili unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa na mtafiti hupata maelezo mazuri kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti. Mbinu hii inaruhusu unyumbukaji katika mwendelezo wa kuuliza maswali, kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu na kupata taarifa za ziada na za kina zaidi, hususan pale ambapo majibu ya watu wanaosailiwa hayaeleweki (Kothari, 1990 na 2004). Hivyo, mbinu hii ilimsadia mtafiti kukusanya data za kutosha na zilizo yakini zaidi. Katika utafiti huu, usaili wa aina mbili ulitumika yaani, usaili rasmi na usaili usio rasmi. Usaili rasmi ulitumika kwa sababu walichaguliwa wahojiwa ambao walikuwa

wametayarishwa kujibu maswali yaliyokusudiwa kujibiwa, kama vile wanafunzi wa sekondari na wanafunzi wa Chuo Kikuu. Usaili usio rasmi uliandaliwa kwa wahojiwa ambao walihojiwa kwa vikundi kulingana na mahitaji ya utafiti.

Kwa kutumia usaili rasmi seti ya maswali huandaliwa katika mpangilio na maswali huulizwa hatua kwa hatua kufuatana na mpangilio huo (Kothari, 2004). Katika utafiti huu, mtafiti aliandaa maswali ambayo yalikuwa ni maswali ya mwongozo wakati wa kufanya usaili. Maswali hayo yaliulizwa kwa mpangilio wa kufuata hatua kwa hatua kulingana na kundi la wahojiwa. Kila kundi lilikuwa na maswali yake ambayo yalikuwa yameandaliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Hivyo, wahojiwa wote waliulizwa maswali sawa kulingana na maswali ya mwongozo wa usaili yaliyoandaliwa. Usaili ulifanyika kwa wanafunzi wa riwaya wa Chuo Kikuu cha Huria Pemba, walimu wa fasihi hususani riwaya na wanafunzi wa sekondari. Wakati wa usaili mtafiti alitumia karatasi na kalamu kuandika mambo muhimu katika mazungumzo baina yake na wahojiwa. Data zilizohifadhiwa katika zana hizo zilimsaidia mtafiti katika uchambuzi Hivyo, kwa kutumia mbinu hii, mtafiti aliweza kupata data ambazo zilimuongoza katika kufanya majumuisho ya data za utafiti wake.

### 3.4.3 Zana za Utafiti

Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa kutumia zana ya hojaji.

### 3.4.4 Mbinu ya Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu hii huhusisha uandaaji wa maswali ya hojaji ambayo hutumwa kwa muhusika kwa maombi ya kumtaka mtafitiwa kujibu maswali

yaliyomo hatimaye kurudisha kwa mtafiti. Hojaji huhusisha orodha ya maswali ambayo huwekwa katika mpangilio maalumu. Kothari (1990) anasema kuwa, katika kiwango cha mahojiano ya msingi ya utafiti usio wa kitakwimu, undani na taarifa za ziada kuhusu hisia, uzoefu na maarifa ya wahojiwa hujionyesha vyema kupitia maswali funge. Hivyo, katika utafiti huu, mtafiti aliandaa maswali ili kuwapa uhuru na nafasi wahojiwa kujibu kwa uhuru na kuelezea hisia, uzoefu na maarifa waliyonayo juu ya mada husika.

Sababu kubwa ya kuamua kutumia mbinu hii ni kwamba, mhojiwa huwa huru kuelezea hisia, mawazo na maoni yake juu ya jambo fulani kwa uwazi zaidi. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data za kutosha na kwa uwazi zaidi kwa kuwapa wahojiwa nafasi ya kuelezea mawazo, hisia, mtazamo na uzoefu wao. Hivyo kutokana na mbinu hii mtafiti aliweza kupata data za kutosha kulingana maswali aliyoyatoa kulingana na malengo ya utafiti, ambayo yalimuezesha kuchambua data za utafiti kuilingana na malengo yake. Hata hivyo ili kukidhi malengo ya utafiti huu, tuliamua kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi. Mbinu ambayo tuliamini itaibua hisia, mtazamo na maoni ya wahojiwa.

### 3.4.5 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Katika utafiti huu, mbinu ya majadiliano ya vikundi ilitumika kukusanya data za utafiti huu. Mtafiti alitumia majadiliano ya vikundi kwa kuwakusanya wanafunzi wa fasihi katika shule ya Sekondari ya Uweleni, iliyopo Mkoani Pemba. Makundi hayo yalihusisha watu watano hadi saba ambao waliwekwa katika chumba kwa muda tofauti.

Kwa kila kundi mtafiti alifanya majadiliano ya dakika ishrini na tano hadi dakika thelathini na tano.

Sababu kubwa ya kuamua kutumia mbinu hii ni kwamba, katika majadiliano mtafiti alilenga kupata maoni, mtazamo na mielekeo juu ya riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.* Kwa hivyo, mbinu hii ilitufaa katika utafiti huu na ilitusaidia kupata data kuhusu ufasihi simulizi uliomo katika kazi hizo za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

### 3.4.6 Hojaji

Kwa mujibu wa Kitula (2010), hojaji huandaliwa kwa lengo la kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa watafitiwa. Aidha, Kothari (1990), anasisitiza kuwa hojaji iliyoandaliwa vizuri ni ile ambayo maswali yake yamepangwa katika mtiririko maalumu ili mtafitiwa aweze kujibu maswali hayo kwa urahisi. Mtafiti alichagua njia ya hojaji kwa sababu njia hii huweka ulinganifu wa majibu yatakayotolewa na watafitiwa wote. Njia hii ilirahisisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa watafitiwa wengi tena kwa muda mfupi. Vilevile njia ya hojaji ilirahisisha kazi ya kufanya majumuisho ya majibu yaliyopatikana. Hojaji za maandishi ziliandaliwa kwa ajili ya walimu wa sekondari na chuo Kikuu Huria, wanafunzi wa fasihi na waliosoma kazi za mtunnzi ambao wanaoishi maeneo ya Mji wa Mkoani pamoja na Chake Chake Pemba.

## 3.5 Matini

Matini tulizozizungumzia hapa ni matini za riwaya ya *Adili na Nduguze na Wasifi wa Siti Binti Saad*. Mtafiti alitumia matini hizi kama chanzo cha data za upili kwa sababu katika matini kuna matumizi ya lugha na vipengele vya fasihi simulizi.

### 3.6 Uchambuzi wa Data

Utafiti huu ni utafiti uliotumia sifa za utafiti usio wa kitakwimu. Zipo mbinu mbalimbali zilizotumika kuchambua data za utafiti wa aina hii. Hata hivyo, data ya utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani uchambuzi maudhui na uchambuzi fafanuzi. Ntarangwi (2004) anaelezea uchambuzi maudhui kuwa ni mbinu ya uchambuzi ambayo huziweka mada kulingana na jinsi jamiii inavyohusiana na kazi hiyo katika mila, destuti, silka  pamoja na utanmaduni wa jamii hiyo na kuhusiana na kuihusisha na kazi hiyo moja kwa moja.

Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba ilitusaidia kuweka maana zote zinazohusiana kutokana na data za dodoso na usaili ili kutoa mawazo ya jumla kulingana na malengo ya utafiti huu. Kwa upande mwingine, uchambuzi maudhui hutumika kumithilisha data kutoka kwa watu tofauti. Mbinu hii iliteuliwa kutumika kwa sababu ilisaidia kuweza kumithilisha vipengele vya fasihi simulizi  ili kubainisha jinsi vinavyochangia kuibua riwaya za Kiswahili. Katika kazi za msanii na hatimaye kupata majumuisho ya matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi vinavyotumiwa na msanii wa riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

Katika uchambuzi wa data za utafiti huu mtafiti alifanya yafuatayo:

(1) Kuchambua vipengele vya fasihi simulizi katika Riwaya ya *Adili na Nduguze*.

(2) Kuchambua vipengele vya fasihi simulizi katika Riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

(3) Kufafanua vipengele vya fasihi simulizi katika kitabu cha *Adili na Nduguze,* kwa kuhusisha dhamira na kufasiri matokeo kwa kuweka majibu yanayofanana na kuhusiana katika kundi moja.

(4) Kufafanua vipengele vya fasihi simulizi katika kitabu cha *Wasifu wa Siti Binti Saad*, kwa kuhusisha dhamira na kufasiri matokeo kwa kuweka majibu yanayofanana na kuhusiana katika kundi moja.

(5) Kufasiri na kuchambua majibu ya mawsaili (usaili, dodoso na majadiliano) na kuweka majibu yanayofanana.

(6) kuzifasiri na kuchambua data za maktaba na kuzijadili kwa kutumia maelezo, namba na chati.

**3.7 Hitimisho**

Sura hii imejadili juu ya mbinu zilizotumika katika kukusanya data za utafiti huu. Imejadiliwa katika sura hii kuwa eneo la utafiti litakuwa ni Pemba na walengwa wa utafiti huu ni walimu wa fasihi, wanafunzi wa fasihi Sekondari, wasimulizi wa hadithi na wasikilizaji. Aidha, sura hii imejadili mbinu za ukusanyaji data ambazo ni mbinu ya usomaji machapisho, usaili, dodoso na majadiliano. Mbinu hizi zilitumika kwa kukamilishana na kujalizana kwa data ilizopatikana iliyotumika kutokana na mbinu moja na nyingine. Katika sura hii imejadiliwa kuwa nadharia ilikayotumika katika uchunguzi na uchambuzi wa data za utafiti huu ni nadharia ya mwingilianomatini.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusiana na mada iliyofanyiwa uchunguzi. Utafiti huu ulilenga kuchunguza ufasihi simulizi katika riwaya za Kiswahili kwa kutumia mifano ya riwaya za Shaaban Robert za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti bint Saad*. Lengo lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi na kuonesha jinsi vipengele hivyo vinavyotumika katika kuibua dhamira za kazi hizo. Utafiti huu umebaini kuwa, riwaya zote mbili zimeandikwa na msanii anayeitwa Shaaban Robert, ambapo msanii huyu anatoka katika mwambao wa Afrika Mashariki katika maeneo ya Tanzania (taz. Chuachua, 2009 na Ponera 2010). Kwa ujumla wa sura hii inajibu maswali mawili ambayo yaliongoza utafiti huu. Kwa hiyo, uwasilishaji na mjadala wa data za utafiti huu umejikita katika maswali hayo. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu vipengele vya fasihi simulizi, sehemu ya pili ni dhamira zilizoibuliwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi na tatu ni hitimisho.

## 4.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Riwaya Teule

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji wa machapisho kwa kusoma, kuchambua na kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya zote mbili. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa, msanii anatumia vipengele vya fasihi simulizi katika utunzi wake. Aidha, mbinu ya dodoso, usaili na majadiliaano ya vikundi

zilitumika kuthibitisha, kujaliza na kukamilisha data za utafiti zilizopatikana kupitia mbinu ya usomaji wa machapisho. Kwa ujumla data zilizopatikana kwa kutumia mbinu hizo, zilithibitisha matokeo ya awali hii ina maana kuwa, matokeo haya hayakutofautiana na matokeo yaliyopatikana wakati wa usomaji wa machapisho. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* zimejengwa kwa kutumia vipengele vya fasihi simulizi. Jedwali lifuatalo linaonesha vipengele vya fasihi simulizi vilivyobainishwa katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

**Jadweli na 3 – Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Riwaya Teule**

| **Na.** | **Kipengele cha Fasihi Simulizi** | ***Adili na Nduguze*** | ***Wasifu wa Siti binti Saad*** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mandhari | √[1] | -[2] |
| 2. | Wahusika | √ | - |
| 3. | Masimulizi | √ | √ |
| 4. | Ushairi | √ | √ |
| 5. | Utani | √ | √ |
| 6. | Semi | √ | √ |

**Chanzo** : Data kutoka Riwaya Teule (Novemba 2014)

Jadweli Na. 3 hapo juu, linadhihirisha kuwa Riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, zimejengwa kwa kutumia malighafi ya fasihi simulizi. Data hiyo inaonesha kuwa, msanii katika *Adili na Nduguze* ametumia vipengele vya mandhari, wahusika, masimulizi, ushairi, utani na semi. Kwa upande wa Wasifu wa Siti Binti Saad msanii ametumia vipengele vyote isipokuwa mandhari na wahusika. Hii ina maana kuwa wahusika waliotumika katika riwaya hii si wahusika wa fasihi simulizi na hata mandhari yake ni ya uhalisia ambayo haina sifa za fasihi simulizi. Kwa ujumla utafiti huu umebaini kuwa, vipengele vya Fasihi Simulizi vimetumika kama mbinu ya kisanii

[1] Alama hii inaashiria kuwa kipengele fulani kimetumika
[2] Alama hii inaashiria kuwa kipengele hakijatumika

katika kujenga Riwaya za Kiswahili. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa, matumizi ya mbinu za fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi ni kuonesha uasilia wa jamii za Kiafrika na fasihi ya Kiafrika katika fasihi andishi. Vipengele hivi vinaonesha kuwa, kuna kuingiliana na kuathiriana kwa mbinu za utunzi wa kazi za fasihi hoja ambayo inasisitizwa na wana nadharia ya muingilianomatini. Utafiti huu umebaini kuwa, vipengele vya fasihi simulizi vinatumika kama malighafi ya utunzi wa riwaya.

### 4.2 Vipengele vya Fasihi Simulizi na Uibuaji wa Dhamira

Moja ya lengo mahsusi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha dhamira zinaziowasilishwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi. Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi utafiti ulibaini kuwa, vipengele vya fasihi simulizi si kwamba vinatumika kama malighafi ya utunzi katika riwaya za Kiswahili hususani za Shaaban Robert bali matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi huwa na dhima maalumu kisanii. Vipengele hivyo hutumika kama mbinu za kisanii zinazobeba dhamira za riwaya hizo. Sehemu ifuatayo inajadili vipengele vya Fasihi Simulizi na dhamira zilizoibuliwa kutokana na matumizi ya vipengele hivyo.

### 4.2.5 Matumizi ya Dhamira katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*

Kipengele cha dhamira pia kimetumika katika kukamilisha kazi ya *Adili Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.* Utafiti umebaini kuwa dhamira zilizotumika ni zile zile za fasihi simulizi. Kwa upande wa *Adili na Nduguze* ni kama ifuatavyo : mandari ya baharini, maweni na majabalini (yameibua dhamira za ubinafsi, uvivu, umasikini), wahusika kama vile Ikibali, Adili na Faraja, Hasidi, na Mwivu (uadilifu, uwajibikaji,

elimu, huruma, upendo, uadui, choyo na wivu), mhusika dhahania/jini/Huria ( Dhamira ya uadilifu na uhuru katika maamuzi), masimulizi (wivu, choyo, na chuki, uongozi mbaya, uongozi bora, ubinafsi, usaliti, elimu na uwajibikaji, ujasiri, na nguvu), ushairi (kuepuka maovu, semi kama vile methali, tamathali ya semi ya takriri (ustahamilivu, mapenzi, majisifu,uadilifu). Katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* vipengele husika na dhamira zake ni (utubora, kujiamini na kutokata tamaa), ushairi (wivu, chuki, dini, heshima, kutenda mema), utani (ukweli, pongezi), na semi kama vileta ta ta methali, takriri (ukweli wa maisha, mafanikio). Uchambuzi wa data umerejelea data za uwandani na mifano kutoka kitabu cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

### 4.2.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi na Dhamira katika *Adili na Nduguze*

Kama tulivyoeleza hapo awali, utafiti huu ulibaini kuwa, vipengele vya fasihi simulizi hutumiwa na msanii katika kuibua dhamira za kazi yake ya fasihi. Sehemu ifuatayo inajadili vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na dhamira zinazoibuliwa kutokana na mbinu ya matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi.

#### 4.2.1. 1 Matumizi ya Mandhari katika *Adili na Nduguze*

Utafiti huu ulibaini kuwa, mtunzi katika *Adili na Nduguze*, ametumia mandhari ya fasihi simulizi kama vile mandhari ya baharini na kuibua dhamira ya ubinafsi. Tazama dondoo ifuatayo;

> (1) *Usiku Adili alipokuwa amelala na jahazi inakwenda mbio kwa pepo za omo, ndugu zake walikuwa macho. Mawazo mabaya hurusha usingizini. Kuzinduka kwake usingizini Adili alijiona amechukuliwa*

*hangahanga. Mmoja alimshika kichwani na mwengine miguuni. Koo yake ilisongwa sana".* (*Adili na Nduguze* Uk. 33)

Mfano namba 1 hapo juu unaonesha kuwa msanii ametumia mandhari ya bahari ambayo yanaibua dhamira ubinafsi. Mandhari ya aina hii ni mandhari ambayo hutumiwa katika masimulizi ya hadithi, visakale na ngano za Kiafrika. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walibainisha kuwa, msanii ametumia mandhari hii kuonesha ubinafsi hali ambayo inasababisha usaliti wa ndugu za Adili kuamua kumtosa baharini ndugu yao ambaye ni mhusika Adili. Mwandishi anaonyesha kuwa Adili, alitoswa baharini kutokana na mali yake mwenyewe. Hii inadhihirisha usemi wa Kiswahili usemao 'Nyuki hutiwa moto sababu asali yake'.

Aidha, mandhari ya mji wa mawe ni mandhari ya fasihi simulizi inaibua dhamira ya uvivu. Tazama mfano ufuatao

> *(2) "Kila barabara aliyopita ilikuwa na watu, Ng'ombe, farasi, Nyumbu, punda na mbwa lakini wote walikuwa mawe matupu. Hofu kubwa ilitamba moyoni mwake kuwa naye asije geuzwa jiwe. Lakini alifarijika kuwa labda ilikuwako katika mji ule, wanyama na vitu vyake kuwa mawe, na kuwa lilikuwa fundisho kwake".* (*Adili na Nduguze* uk 28)

Mfano namba 2 hapo juu unaonesha matumizi ya mandhari ambayo yanaibua na kujenga dhamira ya uvivu. Msanii anaonesha kuwa katika sehemu hiyo kuna rasilimali nyingi lakini watu wote walikuwa mawe matupu. Mawe matupu hapa imetumika kama sitiari inayowakilisha watu wasiofanya kazi wavivu. Kwa kawaida jiwe haliwezi

kufanya kazi na haliwezi kuhama sehemu lilipo. Dhana hii inajenga dhamira ya uvivu pamoja na kuwepo kwa utafjiri mkubwa watu walikuwa hawautumii.

Vile vile utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia mandhari ya jabali kuibua dhamira ya umaskini. Tazama dondoo ifuatayo;

> *(3) "Baada ya safari ya siku moja walifika jabalini. Nahodha aliamuru kutua tanga na kutia nanga. Kisha mabaharia walitakiwa washuke jabalini kutafuta maji kwa sababu jahazini mlikuwa hamna maji hata tone moja".* (*Adili na Nduguze* uk. 22,)

Mfano namba 3 hapo juu unaonesha kuwa, msanii anatumia mandhari ya jabali kuibua dhamira ya umaskini. Hii inadhihirishwa na pale msanii anaposema jahazini mlikuwa hamna maji hata tone. Maneno hayo yanaonesha kuwa, wafasiri hao walikuwa na njaa na kiu kutokana na umaskini uliokithiri katika nchi yao.

#### 4.2.1.2. Matumizi ya Wahusika katika *Adili na Nduguze*

Wahusika kama inavyojulikana ni wawakilishi katika kazi ya fasihi ambao huwakilisha tabia, matendo, hulka na silka kulingana na muktadha halisi wa jamii ambao huambatana na mila na desturi za jamii husika. Wahusika hawa ni wahusika wa kiishara ambao pia huwasilishwa kitabia kulingana na majina yao, ambao vile vile hupatikana katika fasihi simulizi, mfano katika hadithi kama vile Visakale, Visajanja na Vigano.

Mwandishi wa kitabu cha *Adili na Ndguze* ametumia wahusika na wameibua dhamira ya uadilifu na uwajibikaji Mwandishi anasema kuwa;

(4) *"Jioni Ikibali na Adili walipokuwa peke yao mazungumzo juu ya kodi yalianza. Hapakuonekana na upungufu wowote. Hesabu haikuwa kamili tu, lakini ilionyesha ziada vile vile".* (*Adili na Nduguze* uk. 06,)

Mfano namba 4 hapo juu unaonesha kuwa msanii anawapa majina wahusika kulingana na sifa zao, kulingana majina yao, mfano Ikibali kwa maana ya kuwa mtu anayeelekeza mambo fulani na pia ni ujio wa mtu mwenye kazi maalumu inayotakiwa kuchunguzwa. Kwa kutumia majina ya wahusika msani anaibua dhamira ya uwajibikaji kwa kuonesha umuhimu wa kufanya kazi. Dhamira hii inonyesha kuwa kila mtu afanye kazi kulingana na ujuzi ilioupata, na pia ni muhimu kufanya kazi, kwasababu kazi ndio msingi wa maendeleo. Vile vile jina la Adili linaibua dhamira ya uadilifu. Kwa kutumia jina la mhusika Adili msanii anaibua dhamira ya uadilifu katika maisha na jamii. Hapa anaonesha kuwa, kiongozi lazima awe mwadilifu, mnyenyekevu na mwaminifu. Apende kutimiza wajibu wake katika jamii kulingana na kazi yake aliyopewa na wajibu wake katika jamii. Dhamira hii inadhdihirisha kuwa, kazi ndio msingi wa kila kitu katika jamii na ni msingi wa maendeleo kwa jamii yoyote.

Vile vile msanii anatumia jina la Ikibali, kuibua dhamira ya elimu na umuhimu wake katika jamii. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa, majina ya wahusika yametumika kuibua na kubeba dhamira mbalimbali. Wakitolea mfano wa Adili na Ikibali wahojiwa walisema kuwa, wahusika hawa kwa pamoja wamebeba dhamira ya umuhimu wa kutafuta elimu kwa njia yoyote ile, mpaka mtu afanikiwe na kile anachokitafuta kwa kujua jema na lililo baya. Aidha, anatumia mbinu ya safari kuonesha umuhimu wa elimu na sababu ya kuitafuta elimu kwa gharama yoyote ile. Hapa msanii anawatumia wahusika hao na safari yao ya kuitafuta elimu katika maeneo mengine.

Utafiti huu ulibaini kuwa, mwandishi anatumia majina ya wahusika na wahusika wenyewe kuwabebesha dhamira ndani yao. Katika matendo yao, tabia zao na majina yao. Tazama mfano katika dondoo lifuatalo;

> *(5) "Adili alisema manyani manyani walikuwa ni ndugu zake. Baba yao aliitwa Faraja. Faraja alikuwa mtoto wa pacha. Wakati wa kuzaliwa pacha hiyo mtoto mmoja alikufa. Huyu aliyebakia aliitwa Faraja kwa sababu aliwafariji wazazi wake katika msiba wa ndugu yake. Alipokuwa wazazi wake walimwoza mke, yaani mama yao. Mama yao ilichukuwa mimba ya kwanza akazaa mwana aliyeitwa Hasidi. Alichukuwa mimba ya pili akazaa mtoto aitwae Mwivu na kuchukuwa mimba ya tatu akazaa mwana tena aliyeitwa Adili".*
> (*Adili na Nduguze* uk. 14,)

Katika mfano namba 5 hapo juu unaonesha kuwa mhusika mwenye jina la Faraja anaibua dhamira ya faraja na kufarijiana katika kila jambo. Katika matatizo na shida zote ndani ya jamii. Dhamira hii pia inaenda sambamba na dhamira ya huruma na upendo. Kwamba mtu anayetoa faraja kwa mwingine ni mwingi wa huruma na upendo. Kwa upande wa mhusika Hasidi mtunzi anatumia jina la mhusika huyu kuibua dhamira ya uadui na choyo. Uchoyo ni hali ambayo inaonyesha ukosefu wa usawa na haki katika uongozi wa aina yoyote. Aidha, kwa kutumia muhusika Mwivu msanii anaibua dhamira ya wivu. Kwa kutumia mhusika huyu, msanii anaonesha kuwa wivu na uhasidi ni adui wa maendeleo katika jamii. Vile vile ni hali inayonyesha kuwa wivu ukizidi sana kwa kwa kitu chochote huleta madhara katika jamii. Msanii anaonesha kuwa wivu ndio uliowafanya nduguze Adili kumwonea wivu na kumtupa baharini kwa kusudia kumuuwa.

Utafiti huu ulibaini kuwa, msanii katumia wahusika dhahania kwa mfano, mhusika Huria ambaye amechorwa kama jini lakini anawakilisha muhusika ambaye ni hakimu muadilifu katika kuamua kesi kwa kumsikiliza muathirika na aliyesababisha tukio linalojadiliwa. Huria kulingana na mwandishi anatupatia dhamira ya uadilifu na uhuru katika maamuzi. Uadilifu huu unaonekana pale ambapo wahusika wawili, Hasidi na Mwivu walipotenda mabaya na kisha kuhukumiwa na kulingana na makosa yao, walihukumiwa kupigwa pamoja na kufungwa, ndio hukumu waliyopewa walipotaka kumuua ndugu yao Adili. Vile vile kulingana na mwandishi maelezo yanaonyesha kuwa unapoaminiwa na wewe unatakiwa kujiamini, kwasabubu Adili aliwaamini ndugu zake Wivu na Hasdi lakini wao walishindwa kujiaminisha kwa ndugu yao Adili.

#### 4.2.1.3 Matumizi ya Masimulizi katika *Adili na Nduguze*

Utafiti huu ulibaini kuwa, msanii anatumia masimulizi ya kifasihi simulizi katika kuibua dhamira za kazi yake. Masimulizi katika riwaya ya *Adili na Nduguze* yanaibua dhamira mbalimbali kama vile wivu, choyo na chuki, uongozi mbaya, ubinfasi, usaliti, umuhimu wa elimu na uadilifu na uwajibikaji. Tazama mfano ufuatao;

> *(6) "Rai, mfalme wa Ughaibuni, alikuwa mfalme wa namna ya peke yake Duniani, alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia ya watu wengine wa zama zake. Tabia yake ilijigawa katika thuluthi tatu mbalimbali kama ngozi ya punda milia. Kwa thuluthi ya kwanza alikuwa msuluhifu, akapendwa na watu, kwa thuluthi ya pili alikuwa kama Daud akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama, na*

*kwa thuluthi ya tatu alikuwa kama Suleiman akatiiwa na majini”*. (*Adili na Nduguze* uk. 01)

Katika mfano namba 6 hapo juu msanii anatumia masimulizi ya hadithi kuibua dhamira ya kiongozi bora na uongozi bora. Hapa msanii anatuonesha jinsi kiongozi bora anavyoweza kuheshimiwa na kupendwa na watu. Msanii anatumia masimulizi kuibua sifa za kiongozi bora ni yule anayesikiliza mawazo ya wale anaowaongoza.

Katika mfano namba 6 pia tunaona mwandishi akiibua dhamira ya utamaduni. Jamii za pwani ya Afrika Mashariki huamini kwatika viumbe visivyoonekana ambavyo ni majini. Viumbe hawa wamepewa nguvu na uwezo wa ajabu na jamii huamini katika uwepo wa viumbe hao. Kwa hiyo, msanii anatumia wahusika hawa dhahania kuonesha nguvu na uwezo wa kiongozi ambaye pia anapewa heshima na utii wa viumbe hivi dhahania.

Vile vile mwandishi anasema

> *(7) “Kila mahali Huria alipopita, Hunde alifuata Nyayo zake mpaka aligundua alikokuwa, iliendelea hivyo hata kiasi akapigana naye. Alishindwa akakimbia, huria. Huria alipotaka kutembea alijigeuza umbo la mnyama, kila alipojigeuza na yeye alijigeuza vile vile, akanusa harufu yake kama mbwa. Alipojigeuza panya, yeye alikuwa paka, alipojifanya paka, yeye alijigeuza chui, na alipokuwa chui, yeye akawa simba”.* (*Adili na Nduguze* uk. 45).

Masimulizi haya yanaibua dhamira ya ujasiri na nguvu. Hapa msanii anatumia masimulizi haya kuonesha ujasiri, ushujaa na nguvu za mhusika. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walisema kuwa, masimulizi haya yanaibua dhamira ya ujasiri na ushujaa ambao unaonesha uwezo waliokuwa nao wahusika katika kuyakabili mazingira yao.

Masimulizi pia yametumika kuibua dhamira ya elimu kwa mfano Adili aliposema;

> *(8) "Alipogeuka kwa ndugu zake Adili, Rai alionya kama wavivu walijitahidi kuwa hodari, ilikuwa kinyume hodari kuwa mvivu; kama waovu walitaka kuwa wema, ilichukiza wema kuwa waovu; kama masikini walitafuta utajiri, ilikuwa ujinga matajiri kufuja walichonacho; kama mbegu kidogo iliyogeuzwa mchanga ilikuwa uharabu mtu kuuwa ndugu yake; pia ilikuwa aibu kubwa sana kwa wazuri kutenda maovu".* (*Adili na Nduguze* uk. 48)

Katika mfano namba 8 hapo juu, tunaona kuwa, msanii anaibua dhamira ya elimu kwa kutumia mbinu ya masimulizi. Funzo analolitoa Adili katika masimulizi hayo ni kila moja ajitahidi kuwajibika kulingana na elimu aliyonayo na kuitumia elimu hiyo katika kufanya kazi na kuwajibika.

#### 4.2.1.4 Matumizi ya Ushairi katika *Adili na Nduguze*

Utafiti umebaini kuwa msanii ametumia utanzu wa ushairi katika kuibua dhamira za kazi yake. Tazama mfano namba 9 hapa chini;

*(9) Mawe huwa dhahabu*

*Au johari na chuma,*

*Na mtu anapotubu*

*Dhambi yake kukoma,*

*Nishani zake dhahabu*

*Na heshima ya daima.*

*(Adili na Nduguze uk. 48).*

Mfano namba 9 hapo juu unaonesha matumizi ya ushairi katika riwaya. Kwa kutumia mbinu ya ushairi mtunzi anaibua dhamira ya kuepuka uovu. Hapa msanii anaonesha kuwa mtu anapoacha kutenda dhambi hubadilika na kuwa mwema na kuheshimiwa na jamiii. Dhamira hii inajenga umuhimu wa kupatikana kwa amani, upendo na kutokea kwa utulivu katika jamii, na pia huwa ni heshima kwa wale walioomba msamaha baada ya kufanya kosa na kuwa watu bora kulingana na jamii.

#### 4.2.1.5 Matumizi ya Semi *Adili na Nduguze*

Utafiti umebaini kuwa katika kitabu cha *Adili na Nduguze* misemo imetumika kuibua dhamira. Dhamira ambazo zinathibitishwa na maelezo yafutayo;

*(10)* *"Ulimi wake mwenyewe ulimponza"* (*Adili na Nduguze* uk. 11)

*(12)* *"Adili ilitamka kuwa maisha ni safari na Dunia ni matembezi kwa wanadamu"* (*Adili na Nduguze* uk. 15)

*(13)* *"Hakika mtu mwenye kuhesabu mapato yake hafi maskini"* (*Adili na Nduguze* uk. 16)

Misemo yote hiyo inaonyesha jinsi ya maisha baada ya kufa au kitu chochote kina faida na hasara. Hivyo utafiti umebaini kila kiti kina mafanikio na pia kina matatizo. Ustahamilivu juu ya mafanikio ya kitu katika maisha huwa kunastahili ustahamilivu. Dhamira ya ustahamilivu inaonekana ni sawa ma kusema mstahamilivu hula mbovu.

Hali aliyomfanya Adili kusubiri ukweli utokee juu yake na kukosa kufa lakini ni sawa na kusema mwenye kusubiri hajuti hata kidago.

Vile vile dhamira ya ustahamilivu inapatikana pale ambapo mtu anapotafuta kitu kwa muda mrefu bila ya mafanikio na baada ya muda kaweza kufanikiwa, hii ina maana kwamba hakuna kitu rahisi kupatikana. Kila kitu hupatikana kwa shida na huwa kina masharti katika kukitafuta, hakuna kupata kwa urahisi isipokuwa ni lazima kuhangaika. Pia utafiti umebaini kuwa mtu anavyoishi ajuwe kuna siku ataondoka katika jamii anayoishi. Hivyo muhusika yoyote anatakiwa kutenda yalo mema ili yamfae baada ya kuondoka katika ulimwengu kwa kufuata mila na desturi za jamii.

Pia misemo mengine katika kitabu cha *Adili na Nduguze* ni ile isemayo;

> *(14)* *"Mwanaume hakukusudiwa kuwa fahali wa kila mtamba wa kila jogoo, wala mwanamke kuwa tembe wa kila jogoo"* (*Adili na Nduguze* uk. 32)

Kutokana na misemo hiyo, utafiti umeibuwa dhamira ya mapenzi ya kweli. Mwandishi anaonyesha kuwa mapenzi ya kweli ni chanzo cha mafaniko ya kuwepo ukweli na uwazi katika jamii. Mapenzi siku zote ndio muonekano wa mtu uzuri wake na hata awe kiongozi wa ngazi yoyote katika jamii hata ile ya familia, na pia utafiti uliona kuwa, swali la ndoa kuwa ndio taasisi kubwa ya kukuza na kuendeleza utamaduni unaopinga mila na desuri mbaya, kwa mfano kuepusha na maradhi mbali mbali yanayosumbua jamii na hata ulimwengu mzima.

Utafiti ulibaini ya kuwa dhamira ya kujisifu. Kujisifu ni hali ya mtu kufanya jambo ambalo haliwezi kulifanya, anafanya kwasababu aonekane tu. Hivyo kujisifu kwa kujua

kitu sio sababu ya kuweza kutatau jambo lililoikabili jamii. Mfano wa maelezo yafuatayo yanathibitisha hilo;

*(15)* *"Aliudhika akataka kumuonyesha Huria uwezo wake. Na tangu alipotishia hivyo hakumpa nafasi hata ya uzi kupenya tundu la Sindano".* *(Adili na Nduguze* uk. 45*,)*

Vile vile kutokana na lengo la utafiti kwa kutokana na msemo uliotangulia, utafiti umegundua dhamira kujitambua. Kujitambua na hali ya kuwepo kwa tabia ya baadhi ya wale wanaojifanya wanajua baadhi ya vitu, kumbe ni kujionyesha tu kuwa wanajua na kumbe hawajui kama hawajui. Hali inayothibitisha kuwa ajuwaye ni yule asiyetaka kusifiwa na ajuae ni yule anayefanya mambo bila kujisifu. Pia misemo imetumika kuibua dhamira iliyokusudiwa kufikishwa kwa wahusika, waliokusudiwa kupewa kufikishiwa dhamira hiyo. Dhamira inayopatikana kutokana na utafiti ni yale yanayobainishwa na maneno yafuatayo;

*(16)* *Alimwambia mama yake kuwa deni alilowiwa na Adili lilikuwa kubwa sana. Hakudai lilipwe lote lakini alitaka lipunguzwe kama lilivyowezekana. Mjeledi ulimwambia Adili wema wake haukuoza".* (*Adili na Nduguze* uk. 46)

Maelezo hayo yanaonyesha jinsi ya dhamira ya uadilifu. Uadilifu ni hali kufanya jambo kufuata misingi na sheria ya jamii. Hivyo kila mtenda wema huitendea nafsi yake na pia mtenda mabaya vile vile huitendea nasfi yake. Dhamira inaonyesha kuwa "kila mchuma janga hula na wa kwao", hii inamaanisha kuwa yoyote anayefanya kosa huwa haathiriki peke yake bali na jamii yake na pia wema hauozi milele. Hivyo utafiti umebaini kuwa kila mtu analolifanya atalipwa kulingana na kile alichokifanya kwa jamii yake. Vile

vile unapotenda wema basi kama yalivyoonyesha maandishi basi iko siku yatakurejea yale yale, ama kama ni mema au ni mabaya lakini yatatokea na kuathiri kwa ubaya au wema. Ni sawa na Adili baada ya ndugu zake kugeuzwa Manyani, yeye mwenyewe Adili kwa mikono yake aliwaadhibu ndugu zake, ni kawaida ya sharia ni sawa na msumeno kukata mbele na nyuma, haichaguwi alipotoka mtu wala anatoka familia fulani katika jamii. Hali iliyoonyesha kuwa hukumu inayofuata linalotakiwa na jamii, ndio kitulizano kwa jamii pale inapofanyiwa uadilifu sheria katika hukumu.

Kwa upande wa methali katika kitabu cha *Adili na Nduguze*, utafaiti umegunduwa kuwa kuna dhamira imeibuliwa kutokana na methali. Methali ndio moja ya njia ya kufikishia mawazo, fikra, shauku pamoja hisia kulingana na matendo ya jamii. Kulingana na maelezo hayo ni kweli kwamba methali ndio kitu rahisi cha kupelekea dhamira kwa jamii kwa urahisi, utafiti umebaini kuwa methali huwa ni daraja baina mtoaji wa methali na jamii. Hivyo dhamira mbali mbali zinapatikana kupitia methali zilizotangulia kwa ajili ya kuvutia na kufikisha dhamira kwa urahisi. Kwasababu methali hutolewa wakati wowote na ni kitu ambacho hutumiwa sana na wazungumzaji. Dhamira mbali mbali zimeonekana kuwa zimetokana na methali hizo. Dhamira kama ile ya ubinafsi, uchoyo na pia ile ya uonevu. Dhamira hizi zimetumika kuweza kuipamba kazi hii ya fasihi andishi. Hali inayonyesha kuwa kumbe fasihi simulizi ni mali ya jamii na pia ndio inayotoa mchango mkubwa katika kazi ya fasihi andishi.

*(17) "Hasidi na Mwivu hawakujua la kutenda. Atakae makaa ya mgomba hapati kitu ila jivu tupu".*

(Ukurasa wa 50, *Adili na Nduguze*)

*(18) “Walakini Adili aliwashukuru akisema bahari haiweki amana ya kitu kieleacho. Kwa kuwa alielewa ameokoka”.*

(Ukurasa wa 50, *Adili na Nduguze*)

*(19) “Damu nzito kuliko maji. Hasidi na Mwivu walikuwa damu ya Adili”.*

(Ukurasa wa 50, *Adili na Nduguze*)

Maelezo yaliokwisha tangulia yanaonyesha kuwa dhamira ya ubinafsi imetawala miongoni mwa wanajamii. Ubinafsi huu unasababisha kuviza maendeleo ya jamii kutoka hatua moja hadi hatua nyingine ya kimaendeleo. Kwa kawaida kila mtu ni mbinafsi wa nafsi yake lakini utafiti umebaini kuwa ubinafsi ukizidi huwa unaleta hasara miongonimwa wanajamii. Hivyo ubinfasi ndio chanzo kimojawapo kinacholeta mfarakano miongoni mwa wanajamii, kulingana na mila, desturi, silka na utmaduni wa jamii.

Vile vile methali kutokana na riwaya ya *Adili na Nduguze* zimeibuwa dhamira tofauti kulingana na maelezo yafuatayo;

*(20) Kula uhundo kwataka matendo, asiye matendo hula uvundo”.*

(Ukurasa wa 28, *Adili na Nduguze*)

Dhamira ya kujitolea inaonekana kuwepo katika methali iliyopita. Kujitolea kuna namna nyingi, hapa imekusudiwa iwe ya kufanya kazi kwa bidii, na kujiamulia kufanya kazi kwa njia yoyote lakini iwe ile ya halali katika kufuata mila na desturi na maelekezo jamii kulingana na wahusika na matendo yao. Hivyo tunatakiwa tujitolee katika kufanya kazi tuepekane na ile hali kuomba omba ndio mafanakio, lakini kumbe uvvivu hauzai

mwana mwema na pia macho sio kipimo ni kidanganyo cha moyo, maneno ndio yanayoweza kuutengeza moyo au kuharibu moyo, hivyo maneno ni kipimo cha kila kitu kwa mwanadamu. Utafiti umebaini kuwa maneno na matendo mazuri ndio mafanikio katika kila kitu, kwasababu kinachosemwa mdomoni huwa kiko moyoni. Maneno yanatakiwa yasiwe mengi bali yafuatwe na matendo na ndipo tuunapochuma juani na kula kivulini kwa raha. Kwa wale wasiopenda kufanya kazi basi wao watabakiwa na kuomba omba tu ni sawa na uvundo.

### 4.2.2 Vipengele vya Fasihi Simulizi na Dhamira katika *Wasifu wa Siti Binti Saad*

Kama tulivyoeleza hapo awali, utafiti huu ulibaini kuwa, vipengele vya fasihi simulizi hutumiwa na msanii katika kuibua dhamira za kazi yake ya fasihi. Sehemu ifuatayo itajadili vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* na dhamira zinazoibuliwa kutokana na mbinu ya matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi.

#### 4.2.2.1 Matumizi ya Masimulizi katika *Wasifu wa Siti Binti Saad*

Katika kuchunguza matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya ya *Wasifu wa Siti Binti Saad* utafiti huu ulibaini kuwa, msanii ametumia masimulizi kama mbinu ya kisanii kuibua dhamira za kazi yake. Utafiti umegundua kuwa mtindo wa riwaya ya *Siti Binti Saad*, ni masimulizi ya hadithi ya wasifu mwanamke shujaa, ambaye aliishi zamani. Msanii anatumia mbinu ya masimulizi kusimulia habari za sifa, wasifu, na tabia za mwanamke huyo mwenye kipaji ambacho alikitumia katika kuitangaza nchi yake pembe zote za Dunia na kujipatia umaarufu. Tazama mfano ufuatao hapa chini.

(21) *"Nchi hazikuhesabu ubora wa watoto wake, mpaka watoto wake walipokuwa wamepita maisha ya mwili, roho zao zilipokuwa zimevuka Ng'ambo ya pili ambako upeo wa macho haukuweza kufika wala mweto wa mwanadamu haukuweza kusikika, tena baada ya miili yao ilipokuwa imekwisha changanyika na vumbi la ardhi, na thamani yao yote kama viumbe bora ilipokuwa imepotea".* (Ukurasa wa 01, *Wasifu wa Siti Binti Saad.*)

Mfano namba 21 hapo juu unaonesha masimulizi ambayo yaibua dhamira ya utubora na umuhimu wa kutambua utu wa mtu akingali hai. Hapa msanii anaibua tabia ya binadamu ambao hawathamini mchango wa mtu mpaka pale anapokufa ndipo huelewa thamani yake. Wakati wa majadiliano ya vikundi wahojiwa walieleza kuwa mara nyingi watu wenye mchango mkubwa kwa taifa sifa zao huoneka wakati wakiwa wamefariki dunia. Utafiti umebaini kuwa matendo mema ni hesabu baada kuondoka katika jamii, na vile vile, matendo mabaya ni sifa baada ya kuondoka katika jamii aliyoishi mwanajamii katika uhai wake, kulingana na utamaduni wa jamii husika. Mwandishi anaonyesha ubora wa Siti ulijulikana katika Afrika Mashariki baada ya kuaga Dunia, hii inadhihirisha kuwa mtu husifiwa baada ya kuondoka Duniani, ndipo huonekana thamani yake.

Vile vile utafiti umebaini kuwa masimulizi yametumika kuibua dhamira ya kujiamini na kutokata tamaa. Tazama mfano ufuatao;

*(22) "Siti alipotokea katika taarabu katika mara ya pili na baadaye, alionekana na mabadiliko kabisa. Zaidi ya kuweza kuimba*

*alionyesha vile vile madaha na mtindo mpya uliochukuwa watu kwa ghafla ukawatia katika mshangao mkubwa"*. (Ukurasa wa 03, *Wasifu wa Siti Binti Saad).*

Kutokana na maelezo hayo utafiti umebaini kuwepo kwa dhamira ya kujiamini. Wakati wa mahojiano ya vikundi, wahojiwa walibainisha kuwa, ujasiri na kujiamini ndiyo silaha aliyoitumia Siti katika uimbaji wake na kujitangaza duniani kote. Hili linathibitishwa na masimulizi ya mwandishi kuwa Siti alipata mafanikio pale alipoondoa hofu na hii ilimpa umaarufu na kutangaza jina lake duniani kote.

#### 4.2.2.2 Matumizi ya Ushairi katika *Wasifu wa Siti Binti Saad*

Katika riwaya ya *Wasifu wa Siti binti Saad*, utafiti huu ulibaini kuwa, mtunzi ametumia mbinu ya ushairi kuibua dhamira ya kazi yake. Tazama mfano ufutao;

*(23) Siti binti Saad*
*Ulikuwa mtu lini?*
*Ulitoka shamba,*
*Na kaniki mbili chini,*
*Kama si sauti,*
*Ungekula nini?*

(Ukurasa wa 22, *Wasifu wa siti Binti Saad).*

Katika mfano namba 12 hapo juu, msanii anatumia ushairi kuibua dhamira ya wivu na chuki. Hapa msanii anaonesha jinsi Saad alivyopigwa vita na watu ambao walimuona kama si mwimbaji bora kwa sababu ya wivu na chuki walizokuwa nazo dhidi yake. Katika shairi hili tunaona kuwa Siti alidharauliwa kwa sura yake na pia alidharauliwa kwa umaskini wake, isipokuwa alisifiwa kwa sauti yake. Umasikini wake unaonekana

kuwa sio tatizo bali ni miongoni mwa utamaduni wake katika mavazi ya kuvaa kaniki na miguuni kuwa hana hata kiatu, dharua hii ni hali ya baadhi ya watu kudharau sehemu moja na kuitukuza sehemu nyengine. Swali lilosababisha kupatikana kwa jawabu ambalo lilijibiwa kama ifuatavyo;

*(24)* *Si hoja uzuri*
*Na sura jamali*
*Kuwa mtukufu*
*Na jadi kubeli,*
*Hasara ya mtu.*
*Kukosa akili,*
(Ukurasa wa 29*, Wasifu wa siti Binti Saad*)

Aidha, kwa kutumia ushairi mtunzi anaonesha majibizano baina ya Siti na maadui wake. Mtunzi anatumia mbinu ya ushairi kuibua dhamira ya elimu na kujitambua. Hapa msanii anaonesha kuwa elimu na kujitambua kiakili na kiutamaduni ndiyo silaha ya ushindi katika mapinduzi yoyote kwa mtu binafsi ama jamii nzima.

Vile vile, utafiti huu ulibaini kuwa katika majibizano hayo ya kishairi msanii anaibua dhamira ya imani ya dini. Tazama mfano ufuatao;

*(25)* *Sikusudi langu*
*Kuvunja utani,*
*Enyi walimwengu,*
*Mwajua yakini,*
*Apendalo Mungu,*
*Haliwezekani.*

(Ukurasa wa 30, *Wasifu wa siti Binti Saad*)

Katika mfano namba 25 tunaona majibu ya Siti kwa madui zake. Hapa msanii anatumia mbinu ya ushairi kuonesha imani ya dini na kuwepo kwa nguvu na uwezo wa Mungu katika maisha ya binadamu. Imani ambayo alikuwa nayo Siti kuwa kila linalomfika binadamu ni mapenzi ya Mungu. Siti alijitambua na kujua yeye ni nani na ana hadhi gani kwa jamii, pia kwa Muumba wa Ardhi na Mbingu na vilivyomo. Pia utafiti umebaini kuwa kutokana na tajriba ya maisha kila mwanajamii ana kipaji fulani alichonacho, ambacho amepewa na muumba wake.

Mbinu ya ushairi pia imetumika kuonesha heshima na tuzo ya ushindi. Tazama mistari ifuatayo;

*(26)* *Siti wa sitiwa*
*Na amaarufu,*
*Na wingi wa haya*
*Na ujamilifu,*
*Pokea hidaya*
*Ingawa dhaifu.*

(Ukurasa wa 32, *Wasifu wa siti Binti Saad*)

Katika mfano namba 15 hapo juu, msanii anaibua dhamira ya heshima na tuzo. Hapa msanii anaonesha kuwa, kila mwenye kufanya jitihada ya kazi yoyote hupewa heshima na tuzo ya jitihada zake na mafanikio yake. Dhamira hii ina lengo la kufunza jamii kuthamini mchango wanayoitoa wanajamii katika kujenga na kuitambulisha jamii kwa jamii zingine duniani.

Katika kielelezo 27 vile vile dhamira ya kuombeana mema imejitokeza. Utafiti unalithibitisha hili kwa kupitia shairi lifuatalo;

*(27)* *Umetoka ushiridu*
*Dua ladhaa adhima,*
*Kurejea Al Amiri*
*Sultani muwadhama,*
*Jamii twamshukuru*
*Mola Haya El Kiyama,*
*Astahiki salama*
*Maulana Al amiri.*

*Bwana ulipondoka*
*Raia tuliinama,*
*Sote tulidhoofika*
*Tulihadhiri jasama,*
*Nasasa umefika*
*Mwili utarudi nyama,*
*Astahiki salama*
*Maulana El Amiri.*
(Ukurasa wa 38 nz 39, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

Utafiti umebaini kuwa katika shairi hili inaibuka dhamira ya kutenda mema. Mwandishi anaonyesha kuwa iliyeombewa duwa, ilitenda mema, kuwapenda na kuwathamini wenzake na yeye alistahili kuombewa dua kutokana na aliyoyatenda. Utafiti umebaini

pia sio jambo zuri kuomba dua mbaya kwa wengine. Hii inamaanisha kwamba wema hauozi na hata ukioza hauwezi kuchakaa, kwasababu mtenda mema hutendea nafsi yake na pia mtenda maovu huitendea nafsi yake. Wema hauozi na uovu hauchakai ila kwa kuomba radhi.

#### 4.2.2.3 Matumizi Utani katika *Wasifu wa Siti Binti Saad.*

Kwa upande mwengine utafiti ulibaaini Mazungumzo (Matani) yalitumika kuibua dhamira. Dhamira ni sawa na zile zilizotumiwa na fasihi simulizi, lakini zimetumika katika kazi *ya Wasifu wa Siti Binti Saad.* Matani katika kielelezo 28 ni kuwa mwandishi ametumia kwa ufundi mkubwa, kiasi ambacho utafiti umebainu kuwa mtunzi Shaaban Robert kuwa alikuwa fundi mkubwa katika kuipamba kazi yake kwa kutumia lugha. Haya yanajibainisha kwa kuangalia maneno yafuatayo;

*(28)* *Siti binti Saad*
*Ulikuwa mtu lini?*
*Ulitoka shamba,*
*Na kaniki mbili chini,*
*Kama si sauti,*
*Ungekula nini?*
(Ukurasa wa 22, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

Maelezo yaliyopita, yaliyowasilishwa kwa muundo wa shairi yanaonyesha kuwa muhuska Siti alikuwa anabishana na kuzungumza na mtu ambaye alifanya matani na Siti, kutokana na utani wa kijadi. Ndipo utafiti ulipobaini Dhamira ya matani. Matani yaliibuka na kuonyesha uhalisia wa mambo yaliyopo katika jamii. Ama kwa maumbile

yake mabaya, sura yake, tabia yake, umasikini na hata eneo alilotoka. Hali ambayo inaonyesha matani fulani baina ya watani wawili wanapokutana katika matani yao ya kimila, kutokana na utamaduni wao na jinsi makabila hayo yanavyofanana na pia kutofautiana kwa hali tofauti. Hivyo kulingana na malengo ya utafiti tunapata dhamira ya utamaduni. Dhamira inasema kuwa matani ndio msingi mkuu wa kujenga udugu baina ya pande mbili zinazohasimiana, pia matani ndio kitu kinachojenga upendo na urafiki miongoni mwa wanajamii miongoni mwao. Kwani unapotaja sifa na utamaduni wa jamii fulani huwa sio ila bali sifa kulingana na tamaduni za watu fulani. Kwani kutaja kivazi na tabia na hulka za mtu, huwa unataja sifa za kabila fulani. Hiyo huwa ni sifa na utambulisho wa kabila fulani.

Vile vile katika kielelezo 29 kinachofuata, dhamira ya ukweli wa mambo unayoambiwa, utafiti unalithibitisha hili kupitia kipande cha shairi kinachosema;

*(29)* *Si hoja uzuri*
*Na sura jamali,*
*Kuwa mtukufu*
*Na jadi kubeli,*
*Hasara ya mtu*
*Kuokosa akili.*
(Ukurasa wa 29, *Wasifu wa siti Binti Saad*)

Kutokana na kipande hicho utafiti umebaini kuwa mazungumzo au malumbano yaliendelea baina ya pande mbili zenye kutaniana baina yao. Dhamira ya ukweli ndipo ilipoibuliwa. Dhamira ya Ukweli ni hali ya kuwa, ukweli unatakiwa kuzungumzwa juu

ya hali ya mwanajamii ya kuwa hatopata umaarufu kwa sura yake, kuwa na nasabu bora au hata kutoka kabila lilobora zaidi ya mwenzake, kwasababu hili hutofautisha kwasababu ya wanajamii kujuana. Pia utafiti umebaini kuwa mwanajamii ambaye hana akili ndiye ambaye atafikwa na kupatwa na taabu, lakini kwa mwenye akili anaweza kufanya analolitaka kilifanya tena kwa manufaa kabisa, isipokuwa kuweka mikakati juu ya jambo hilo, kulingana na jamii fulani.

Dhamira hii ya ukweli, inasisitiza juu ya kuwa mkweli wakati wowote wa maisha kulingana na sifa ya kitu kilivyo unatakiwa kutopotosha, kwani inawezekana kuleta mapambano dhidi ya wanajami na kwasababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe, kwasababu ukweli siku zote ni wenye kujenga, na wala hauwezi kubomoa. Msema kweli ndiye mpenzi kwa viumbe wenzake na msema uwongo huchukiza kwa wenzake. Malumbano (Matani) yaliendelea tena na kuibuliwa kwa dhamira kuomba radhi. Kuomba radhi juu ya kitu au jambo unalotaka kulisema kabla kulisema jambo hilo, uthibitisho wa hayo ni kilelelezo 30. Kama ifuatavyo;

*(30)* *Sikusudi langu*
*Kuvunja watani,*
*Enyi walimwengu*
*Mwajua yakini,*
*Apendalo Mungu*
*Haliwezekani.*

(Ukurasa wa 29, *Wasifu wa siti Binti Saad*)

Kipande hicho cha shairi kinathibitisha kulingana na malengo ya utafiti ya kuwa uzuri wa kitu unapotaka kusema basi ni lazima kuomba radhi mwanzo ndio uendelee kusema

kitu fulani na ndio utaratibu mzuri wa maisha, sio kuomba msamaha baada ya kufanya jambo. Unatikwa kuomba radhi kabla ya kufanya jambo inawezekana kukera na kuwa kosa lakini linafutwa na ile samahani ya mwanzo kabla ya kulifanya hilo. Hali inayoonyesha kuibua wa msemo unaosema "*Ashakum si matusi*" hata mzungumzaji alisema neno ambalo halikubaliki basi huwa tayari ameshaomba msamha kwa jambo hilo. Hivyo kila kitu kina utaratibu wake na mipango yake kulingana watu walivyokubaliana kufanya.

Kutokana na kipande cha shairi kifuatacho utafiti umegundua dhamira ya pongezi. Pongezi ni dhamira inayosisitiza kwamba aisyekubali kushindwa sio mshindani. Pongezi hapa ni lie hali ya kukubali kwa yule anayeshindwa ukweli juu ya kushindwa. Baada ya kushindana baina ya wanajamii wawili ni lazima mmojawapo akubali kushindwa, na ndipo panapopatikana ukweli juu ya jambo fualani linaloshindaniwa. Utafiti umegundua kwamba ni lazima kwa wanaoshindana baada ya kupitikana ukweli ni juu ya mmoja kukubali kuwa ameshindwa juu ya hilo, kutokana na kutolewa kwa sifa za kinachoshindaniwa. Mfano hulka, tabia mila na hata desturi. Pia kupeana zawadi ni jambo jema au hidaya baada ya kufanikiwa kwa kitu fulani ndani yake ijapokuwa kitakuwa hakina thamani kubwa lakini atakaepewa apokee hata kama kina upungufu, hili ndilo jambo jema kwa wanaofuata mila na desturi za jamii. Kwani kutunikiwa ni bora kuliko kuomba. Kuomba ni pingamizi katika maisha ya mtu isipokuwa kwa dharura.

#### 4.2.2.4 Matumizi ya Semi katika *Wasifu wa Siti binti Saad*.

Kwa upande wa kitabu cha *Wasifu wa Siti Binti Saad*, utafiti umebaini kuwa, kuna semi ambazo zimetumika kubebeshwa dhamira na kuibua dhamira kwa mitindo tofauti. Methali kama mbinu inayotumiwa na fasihi simulizi kwa kawaida, kulingana na kielelezo 31 na 32 vinavyofuata kuwa methali ni aina moja ya fasihi simulizi, hii inamanisha kuwa baadhi ya methali zimeonekana ndani ya riwaya hii ya *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Methali zinazosema;

(31) “*Asiyeweza kutuumba na kutuumbua hawezi*”.

(Ukurasa wa 23, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

(32) “*Cheka uchafu usicheke kilema*”.

(Ukurasa wa 23, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

Methali hizo zinaonyesha kuwa ni hali gani mtu anavyotakiwa kwasababu kabla ya kufa basi mtu ajue hajaumbika; vile vile kila kitu kina mwanzo na mwisho wake na kila kitu pia kina muanzilishi na pia mwenye kuweza kukibadilisha umbile lake lilivyo. Methali hizo zinatoa dhamira ya ukweli wa maisha. Na ndipo unapatikana ukweli kwamba kila kitu kina wakati wake na muda wake na kuwa bila ya kulazimisha, kikilazimishwa kinaweza kikaleta madhara katika jamii. Hivyo kila kitu kinaweza kubadilika na kuweza kuleta sura nyingine kuliko kilivyokuwa hapo mwanzo.

Vile vile, kwa upande wa misemo iliyopatikana katika kitabu cha *Wasifu wa Siti Binti Saad*, inathibitisha kuibuliwa kwa dhamira kama ifuatavyo;

*(33)* “*Siti alikuwa si mmoja wa wahuni waliozoea kutoroka kwao wakakimbilia katika miji kukaa kama chaza, au kama kupe na mkia wa ng’ombe”.*

(Ukurasa wa 13, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

Methali katika kielelezo 33, zinatupatia dhamira ya mafanikio. Mafanikio katika maisha ni dhamira inayoonyesha kuwa mafanikio yanapatikana kwa njia moja ya kuwepo na kuwasikiliza wazee na kukaa nao pamoja, hii ni sababu ya mafanikio, wote ambao wamekwenda kinyume na wazee wao au kuwakimbia na wakakimbilia mijini basi wameshindwa kupata mafaniko yaliyo bora kulingana na silka, desturi, silka na utamaduni wa jamii husika. Hii inamaanisha kukimbia tatizo sio kusuluhisha tatizo bali ni kuzidisha matatizo zaidi, kila kitu kinaweza kisiwe pale unapotaka kukifanya, kinaweza kukupa tabu pale ambapo una shida nacho, vile vile jambo baya linaweza kutokezea wakati wawote katika maisha, isipokuwa ni kujipanga katika kukitatua kitu hicho kwa uangalifu na kwa umakini wa hali ya juu, kwa hali ya kuwasikiliza wazee na jamii kwa ujumla. Vile vile Mafankio kwa kawaida ni ile hali ya kupata kile unachotaka na kutatua shida iliyokabili. Kupata na kukosa ni hali pia ya mafanikio katika maisha kwani kukosea ndio njia ya kujifunza na kukijua unachojifunza, lakini jamii ndiye mwalimu wa kwanza katika maisha, mtu hujifunza kutokana na makosa yaliyomkabili kutokana na silka, desturi na utamaduni wa jamii. Hali inayothibitisha kuwa mafanikio hayapatikani ispokuwa kuwasikiliza wakubwa katika jamii, kulingana na jamii inavyotaka.

Semi nyngine ni ile tamathali ya semi ya takriri, takriri inayoonekana hapa ni ile inayoenyesha msisitizo ni ile inayoenyesha msisitizo. Dhamira ya namna ya kujifunza inapatikana, kwa kawaida njia moja ya kujifunza ni ile ya kurejea rejea kwa kile unachojifunza ambacho hakijulikani na ndio inayojenga kumbukumbu ya muda mrefu. Hili linathibitishwa pale Adili alipokwenda kutafuta na kujiuliza na kukariri yale

aliyokuwa anayaona, hali iliyomfanya kufanikiwa katika maisha yake. Utafiti umebaini kuwa mojawapo wa njia ya kujifunza ni kukariri kariri unachojifunza

Vile vile katika katabu cha *Wasifu wa Siti Binti Saad*, dhamira ya elimu na umuhimu wake ndipo inapoibuliwa, kutokana na malengo ya utafiti, kwa maneno yafuatayo;

*(34)* “*Vyungu, vyungu, vyungu vizuri nunueni vyungu kwa bei rahisi”.*

(Ukurasa wa 05, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

*(35) “Mwanamke huyu ambaye hakusoma alikuwa na moyo wa kuhifadhi mambo kama umeme. Kisha aliweza kuyakariri baadaye neno kwa neno kwa namna iliyowashangaza kila aliyemsikia”.*

(Ukurasa wa 09, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

(36) *“Kwa kadri ya sauti ya kinanda ilivyokuwa nzuri, lakini ile ya mwanadamu ilikuwa bora. Hilo lilimfanya Siti kuwa kama Johari katika jumui ile”.* - (Ukurasa wa 10, *Wasifu wa Siti Binti Saad*)

Marudio hayo ya maneno yanaweza kuleta mafanikio ya aina yoyote, rejea kielelezo 34, 35, na 36 itakapokuwa yamefuta mila, desturi na utamaduni wa jamii. Mwandishi anasema kujitahidi kwa Siti katika kunadi kwa sauti nzuri na yakubembeleza iliyorudia rudia baadhi ya majina ya vile alivyoviuza ndio iliyomfanya kuhifadhi vitu vingi na kujifunza na kufanikiwa katika maisha. Utafiti unathibitisha kwamba kurejea rejea ni hali moja ya mafanikio katika maisha. Hivyo katika mchakato wa maisha hakuna jipya isipokuwa unapofuata sheria basi mafanikio hutokea kwa uhakika. Hivyo utafiti umebaini kuwa njia rahisi ya kujifunza ni ile ya kurejea rejea kwa kila unachojifunza. Na pia ni njia moja ya kujifunza sio lazima kuenda darasani, hata ukienda kwa watu wa

kawaida unaweza kujifunza tena kwa manufaa, na kuweza kukitumia kitu hicho kwa uzuri wa hali ya juu, kama alivyofanya Siti.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili juu fasihi simulizi ilivyotumika kuiwasilisha fasihi andishi katika kuibua dhamira ndani ya katika kitabu cha *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Imeelezwa kuwa mwandishi anaweza kutumia kipengele chochote kile cha fasihi simulizi kwa ajili ya kufikisha dhamira. Aidha sura hii imejadili kuwa mwandishi anaweza kutumia mbinu mbali mbali za uteuzi wa vipingele vya fasihi simulizi katika ujenzi wa kazi za kifasihi.

Sura hii imejadili kuwa msanii yoyote anaweza kuibua dhamira kutokana na kipengele chochote cha fasihi simulizi, hii inatokana na ukweli kwamba msanii yoyote anatoka katika jamii fulani, yenye kuonyesha historia yake, itikadi, uchumi, siasa, mambo ya kijamii, siasa, uchumi na utamaduni. Hivyo basi ni dhahiri kuwa jamii yoyote ina utamaduni wake na jinsi wanavyotumia baadhi ya mambo yao katika kupeleka dhamira kwa jamii kulingana na mahitaji yao.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.1Muhtasari

Utafiti huu ulilenga tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Shaaban Robert kwa kuangalia vipengele vya Fasihi Simulizi ndani ya riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* Kuchunguza ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert kwa kutumia mifano ya riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad,* ili kuona ni jinsi gani msanii huyo anatumia vipengele vya fasihi simulizi kama mali ghafi ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Vile vile kubaini jinsi mtunzi huyo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na namna mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira za riwaya hizo. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo yalijibiwa na maswali mawili. Malengo hayo ni; Kubaini vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* na kubainisha dhamira zinavyowasilishwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya za *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

Tatizo la utafiti huu limetokana na uelewa wa mtafiti baada ya kupitia mapitio mbalimbali na kubaini kuwa hakukuwa na utafiti wa kina ambao umejikita katika kuchunguza na kubainisha vipengele vya fasihi simulizi ndani ya fasihi ya fasihi andishi

kwa kutumia nadhari ya mwingilianomatini katika kazi za riwaya. Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni, kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, ili kubaini jinsi vipengele vipi vya fasihi simulizi vilivyotumiwa na mtunzi kama mali ghafi ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili. Hivyo utafiti huu umetumia nadharia ya mwingiliano matini katika kuchunguza, kuchambua, kubainisha na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

Katika utafiti hii mbinu za utafiti zimejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Katika sura hiyo, imebainishwa kuwa eneo la utafiti huu ni Dar es salaam (Chuo Kikuu Huria) na Pemba (Zanzibar). Vile vile kutokana na maeneo hayo ilikuwa rahisi kuwapata watu ambao waliwahi kuziangalia kazi zake, kwa kuandika makala au kuzifanyia utafiti. Kwa hiyo tulitegemea kupata data za kutosha. Kwa upande wa Pemba itakuwa rahisi kupata data za mwandishi wa kitabu cha *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad*, kwasababu vitabu hivi viliwahi kutumiwa mashuleni na bado vinatumika na pia watu wa kawaida wanaendelea kuvisoma. Hivyo, Dar es Salaam na Pemba ndio maeneo tuliyoyaona kuwa ni muhimu na kufaa kukamilisha utafiti huu.

Walengwa katika utafiti walikuwa ni wanafunzi wa umahiri katika fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria waliteuliwa kwa kigezo kuwa ni wanafunzi wanaosoma fasihi, wana maarifa ya nadharia za uchambuzi wa kazi za fasihi na pia wana ujuzi na maarifa katika matumizi ya nadharia na mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi. Vile vile kigezo cha kuwa wanafunzi hawa wanasoma riwaya kwa Kiswahili kililifanya kundi hili kuwa ni rasilimali ya kutosha katika utoaji wa data za utafiti huu.

Walimu na wahadhiri wa fasihi wa muda mrefu ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wanaofundisha kozi ya fasihi, wana ujuzi na maarifa ya kutosha katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa jumla.

Kwa upande mwingine, Walimu wa fasihi wa muda mrefu ni kundi muhimu katika utafiti huu kwa sababu wao ndio wanaofundisha kozi ya fasihi, wana ujuzi na maarifa katika nadharia na vitendo kuhusu fasihi ya Kiswahili na uhakiki wa kazi za fasihi kwa jumla. Vile vile uliwahusisha wazee na vijana wanaoishi nje ya eneo la Mkoani – Pemba, wazee ambao ni kawaida hutamba hadithi kwa vijana na pia vijana ambao hutolewa hadithi za kale, ambao huwa na uzoefu wa kutoa hadithi na wanosimuliwa kuweza kuhifadhi hadithi hizo na kusimulia wenzao.

Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu nne ambazo ni mbinu mbinu ya usaili, mbinu ya majadiliano ya vikundi, Mbinu ya Dodoso na Mbinu ya usomaji wa machapisho ilikuwa ni mbinu kuu ambayo iliyotusaidia kuchambua riwaya zote mbili na kubainisha mbinu ya mwingilianomatini ilivyotumika katika riwaya hizo. Vilevile mbinu ya dodoso, usaili na majadiliano ya vikundi zilitumika kama mbinu jazilizi ambazo zilitumika kujaliza data zilizopatikana kutoka katika mbinu kuu. Uchambuzi wa data za utafiti huu umefanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui. Utafiti huu umetumia mbinu zisizo za kitakwimu katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafi.

Kulingana na malengo ya utafiti huu maswali mawili yalijibiwa, ambayo yalitokana na malengo mahususi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu ni kama ifutavyo. Swali la kwanza lililenga kubaini matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*, kwa kutumia mbinu ya mwingilianomatini, vipengele hivi vimeonyeshwa katika jadweli nambari (2.). Aidha, Kubainisha dhamira zinavyowasilishwa na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya za *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad*. Vipengele hivyo vimeonyeshwa katika jadweli nambari (3).

Utafiti huu umebaini kuwa riwaya zote matokeo ya mapokeo simulizi ambayo msanii aliyapata kuhusu visakale vya fasihi simulizi ya Kiswahili. Masimulizi yametumika katika viatabu vyote viwili vya Shaaban Robert: *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa matini zote ni matokeo ya mapokeo simulizi ya visakale vya fasihi ya Kiswahili. Pamoja na kuwa zote zimetokana na masimulizi lakini matini hizo zinatofautiana katika matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika misingi na kanuni za utunzi. Hii ina maana kuwa, *Adili na Nduguze* na masimulizi ya visakale wakati *Wasifu wa Siti Binti Saad* msingi wake wa kutungwa kumsimulia mwanamke aliyekuwa maarufu Afrika Mashariki pamoja na Dunia ambaye alikuwa ni Siti Saad, na aliishi Zanzibar katika uhai wake.

Kwa ujumla utafiti huu uligundua kuwa, riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* zinafanana katika vipenhele vya fasihi simulizi ijapokuwa havikutumika sawa sawa katika kuibua dhamira.

Halikadhalika riwaya hizi zimetungwa na mtunzi yuleyule, hivyo hiyo huweza kuwa ni miongoni mwa sababu zinazoleta mfanano wa karibu katika matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi. Hii ni kutokana na kuwa mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wake Utafiti huu ulibaini kuwa, mwingilianomatini ni mbinu ya utunzi wa Shaaban Robert kwa sababu mtunzi huyu anatumia fasihi simulizi ndani ya riwaya. Aidha, utunzi wake umedhihirisha kuwa ni matokeo ya athari ya mapokeo aliyoyapata kuhusu fasihi simulizi za Kiafrika hususani visakale. Utafiti huu unamtaja Shaaban Robert kama mwanamwingilianomatini ambaye anadhihirishwa na utunzi wa kazi zake za fasihi. Hivyo, mwingilianomatini ndiyo unampa upekee katika utunzi wa vitabu vyake.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu unahitimisha kuwa Shaaban Robert anatumia mwingilianomatini katika utunzi wake kwa kuingiza matini za fasihi simulizi katika utunzi wa riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Katika riwaya zote mtunzi ameingiza vipengele vya fasihi simulizi ambavyo ni matokeo ya masimulizi na mapokeo ya visakale vya fasihi simulizi ya Kiswahili. Hii imetuthibitishia kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wa kazi zake za fasihi.

Halikadhalika iligunduliwa na utafiti huu kuwa, mtunzi ameathiriwa na mapokeo simulizi ya fasihi simulizi, kwani riwaya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya ukweli katika Afrika. Hii inatokana na mtunzi kuchota malighafi yake ya kutungia riwaya hizi kutoka katika masimulizi hayo ya kimapokeo ya kusikia nayle yaliyotoka katika kinywa cha msimuliwaji wa kisa. *Adili na Nduguze* inatokana na

mapokeo simulizi ya kisakale cha ngano za wasafiri, na *Wasifu wa Siti Binti Saad* ni matokeo ya kisa cha kweli kilichowahi kutokea katika jamii ya watu Wazanzibar.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu unahitimisha kuwa Riwaya ya *Adili na Ndguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* ni Riwaya zinazotaka katika jamii yenye utamaduni mmoja. Utafiti huu, unapendekeza tafiti nyengine zifanywe katika kuchunguza ufasihi simulizi katika tanzu nyengine za fasihi andishi kama vile tamthiliya na ushairi. Hili litasaidia kuibua namna vipengele vya fasihi simulizu kama malighafi fasihi andishi.

## MAREJELEO


Balisidia, M. L. (Bi Matteru), (1987) "*Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*": *Mulika* 19. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (Toleo la Pili - 2). Oxford: Oxford University.

Chuachua na wenzake (2009). *Shaaban Robert*: *Visa na Ukoloni, Katika Mulika*. TUKI: Dar-es-salaam.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI): Chuo Kikuu Dar-es-salaam: Dar-es-salaam.

Kenguru, P.J.M. (2013). Fasihi Simulizi katika kazi ya Utu Bora Mkulima, (M.A Kiswahili), Chuo Kikuu cha Nairobi Kenya, Nairobi

Kihore Y.M (1996). *Kozi ya Maandalizi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar-es Salaam, Tanzania.

Kitula, M. (2010). *Research Methodology for Postgraduate Students*. The Open University of Tanzania: Dar-es-Salaam.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*. Paulines Publication Africa: Kenya.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, R.C. (2004). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited, Publishers.

Masebo J. A na Nyangwine (2004). *Nadharia ya Fasihi Kidato cha (5) na Sita (6)*. Afro Plus Industries ltd .Dar-es Salaam: Tanzania.

Mateeru, M. L. (1976). *Fani ya Hadithi na Riwaya*: *Makala katika kioo cha Lugha*. Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam: Dar-es-salaam, Tanzanai.

Msokilie, B. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*. Dar-es- salaam University Press: Dar-es-salaam.

Mulokozi M.M (1996). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar-es Salaam Tanzania.

Mulokozi M.M (2002). *Tenzi Tatu za Kale*. TUKI: Dar-es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi: Katika Mulika 21*. TUKI: Dar- es Salaam.

Mung'eri, O. B. (2000). *Utetezi wa Maandishi katika Fasihi*: *Nadhariya ya Shaaban Robert, Ripoti ya Tasnifu*. Chuo Kikuu Nairobi: Nairobi, Kenya.

Mwai, W. na Ndungo, W. (1991). *Kiswahili Studies*: *Part Two*. Nairobi: University of Nairobi.

Ndugo C. M na Wafula R.M (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi (Kiswahili part III).* The College of Education and External Studies: Nairobi.

Ndugo C.M. na Wafula R.M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. University of Nairobi: Kenya.

Ndungo, W. C. na Mwai, R. (1991). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Nairobi: Nairobi, Kenya.

Nkwera F.M.V (1979). *Sarufi na Fasihi*: *Sekondari na Vyuo*. Dae-es- salaam: Tanzania Publishing House.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Augustana College: Rock Island.

Ponera, A. (2010). *Athari za Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Dodoma*. Dododoma: Tanzania.

R, Shaaban (1951). *Adili na Nduguze*. Macmillan Publisher: London.

R, Shaaban (1991). *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Mkuki na Nyota Publisher: Dar es Salaam, Tnzania.

Ruhumbika, G. (2003). "*Tafsiri za Fasihi za Kigeni Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili."Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III (2003).* TUKI: Dar-es-Salaam.

Sengo T.S.Y na Kiango S.D (1977). *Hisi Zetu*. TUKI: Dar-es salaam, Tanzania.

Sengo, T. S. Y. (1975). *Shaaban Robert*: *Uhakiki na Maandishi* Yake. Foundation Books: Nairobi.

Senkoro, F. V. (1976). *Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili*. TUKI: Dar-es-salaam.

Senkoro, F. V. (1982). *Fasihi*. Press Publicity Centre: Dar-es-salaam.

Taib, A. H. (2008). *Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili.* CHAKAMA: Dar-es-salaam.

Taib, A. H. (2009). *Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi. Katika Mulika.* TUKI: Dar-es-salaam.

TAKILUKI (1981). *Hapa na Pale*. TAKILUKI: Zanzibar.

TUKI (1985). *Journal of Institute of Kiswahili Research*. TUKI: Dae-es- salaam.

TUMI (1988). *Kiswahili Sekondari*. TUMI: Dae-es Salaam.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Phonex Publisher Limited: Nairobi, Kenya.

## KIAMBATISHO Na. I

## MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WANAFUNZI WA FASIHI, WA CHUO KIKUU NA WALIOSOMA KAZI ZA MTUNZI

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze*** na ***Wasifu wa Siti binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

1. Unadhani ni mbinu gani za kimtindo zinazotumika katika kukamilisha riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad*?
2. Unafikiri mtunzi wa riwaya anaweza kutumia mbinu za kafasihi katika kuunda riwaya zake? Toa sababu.
3. Je, ni mbinu anazozitumia zinaweza kuibua dhamira? kwa nini?
4. Je, maisha ya mtunzi huyu, tajriba yake, uzoefu na imani yake zinaathiri kazi zake ya riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO Na. I1

## MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WASIMULIA HADITHI PAMOJA NA WASIKILIZA HADITHI

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze*** na ***Wasifu wa Siti Binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

1. Unadhani ni mbinu gani za kimtindo zinazotumika katika kukamilisha riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*?
2. Unafikiri mtunzi wa riwaya anaweza kutumia mbinu za kafasihi katika kuunda riwaya zake? Toa sababu.
3. Je, ni mbinu anazozitumia zinaweza kuibua dhamira? kwa nini?
4. Je, maisha ya mtunzi huyu, tajriba yake, uzoefu na imani yake zinaathiri kazi zake za riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATISHO Na. II1**

**MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI WALIMU WA FASIHI**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

1. Unadhani ni mbinu gani za kimtindo zinazotumika katika kukamilisha riwaya ya *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad*?
2. Unafikiri mtunzi wa riwaya anaweza kutumia mbinu za kafasihi katika kuunda riwaya zake? Toa sababu.
3. Je, ni mbinu anazozitumia zinaweza kuibua dhamira? kwa nini?
4. Je, maisha ya mtunzi huyu, tajriba yake, uzoefu na imani yake zinaathiri kazi zake za riwaya ya *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**KIAMBATISHO Na. IV**

**DODOSO KWA WALIMU WA FASIHI CHUO KIKUU HURIA.**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze*** na ***Wasifu wa Siti Binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

**Maelezo Binafsi**

Jina la mhojiwa………………………………

Umri…………………………………………..

Jinsi……………………………………………

Tarehe…………………………………………

1. Taja na eleza mbinu za kifani zilizotumika katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* vina dhima gani katika kazi hizi za fasihi?

   i. …………………………………………

   ii. ………………………………………….

   iii. …………………………………………….

   iv. ……………………………………..

v. ……………………………………………

2. Ni dhima zinazopatikana kwa mtunzi kutumia vipengele hivyo vya kifani katika riwaya?

   ....................................................................................................................

   ....................................................................................................................

   ..............................

3. Unafikiri ni nini faida ya mwandishi katika kutumia mbinu mbalimbali za kifani katika utunzi wa riwaya hizi?

   (i) ………………………………………………………….

   (ii) ……………………………………………………………..

   (iii)……………………………………………………………..

   (iv)……………………………………………………………………..

   (v) …………………………………………………………………………..

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO Na. V

**DODOSO KWA WANAFUNZI WA KOZI YA FASIHI SEKONDARI**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze*** na ***Wasifu wa Siti Binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

**Maelezo Binafsi**

Jina la Mhojiwa……………………………………

Umri…………………………………………………

Jinsi………………………………………………….

1. Taja na eleza mbinu za kifani zilizotumika katika *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* vina dhima gani katika kazi hizi za fasihi?

    i. ……………………………………………

    ii. …………………………………………….

    iii. ……………………………………………….

    iv. ………………………………………..

    v. …………………………………………….

2. Ni dhima zinazopatikana kwa mtunzi kutumia vipengele hivyo vya kifani katika riwaya?

   ...............................................................................................................................

   ...............................................................................................................................

   ..............................

3. Unafikiri ni nini faida ya mwandishi katika kutumia mbinu mbalimbali za kifani katika utunzi wa riwaya hizi?

   (i) ………………………………………………………….

   (ii) …………………………………………………………..

   (iii)…………………………………………………………..

   (iv)…………………………………………………………………..

   (v) …………………………………………………………………………..

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO Na. VI

**DODOSO KWA AJILI WATU WALIOWAHI KUSOMA KAZI ZA MTUNZI**

Mpendwa Mhojiwa,

Ninafanya utafiti kuhusu **Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza vipengele vya fasihi simulizi vilivyomo ndani ya fasihi andishi. Katika kitabu cha ***Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad***, na kuona ni jinsi gani vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumika kuibua dhamira. Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mhojiwa na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu na si vinginevyo.

**Maelezo Binafsi**

Jina la Mhojiwa……………………………………

Umri…………………………………………………

Jinsi………………………………………………….

1. Taja na eleza mbinu za kifani zilizotumika katika *Adili na Nduguze na Wasifu wa Siti Binti Saad* vina dhima gani katika kazi hizi za fasihi?
    i. …………………………………………
    ii. ………………………………………….
    iii. …………………………………………….
    iv. ………………………………………..
    v. ………………………………………….

2. Ni dhima zinazopatikana kwa mtunzi kutumia vipengele hivyo vya kifani katika riwaya?

.........................................................................................................................

.........................................................................................................................

..............................

3. Unafikiri ni nini faida ya mwandishi katika kutumia mbinu mbalimbali za kifani katika utunzi wa riwaya hizi?

(i) ………………………………………………………….

(ii) …………………………………………………………..

(iii)…………………………………………………………..

(iv)…………………………………………………………………..

(v) ………………………………………………………………………..

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**